Ushuhuda Baharini

Asante, Ndugu Borders.

2 Hebu tuendelee kusimama, kwa muda kidogo tu, tunapoinama kimya mbele za Mungu kwa maombi. Je, kuna haja yoyote, usiku wa leo, ungetaka ijulikane kwa kuinua mkono wako kwa Mungu na kumwomba rehema? Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

3 Baba wa Mbinguni mwenye neema, tunakuja, tena, Uweponi Mwako kwa ajili ya rehema, tukijua ya kuwa Wewe umetuahidi kwamba tutapata rehema, kama tukirehemu, "Wenye rehema watapata rehema." Na kama tumetenda dhambi na kufanya yasiyostahili mbele Zako, Mungu, uturehemu, kwa sababu kwamba tunakupenda na tunakuamini Wewe, Bwana, kwa yote yaliyo ndani yetu.

4 Nasi tunasimama, usiku wa leo, kati ya walio hai na waliokufa, na kuomba ya kwamba utaturehemu na kutuondolea kutokuamini kwetu kwote ili, usiku wa leo, Roho Mtakatifu mkuu apate kufanya kazi ya Mungu miongoni mwetu, na alete uhalisi kwa watu wa ufufuo wa Mwana mpendwa wa Mungu, Bwana Yesu.

5 Jinsi tunavyokushukuru, huko nyuma, jinsi ambavyo hajawahi kutupungukia. Sote tunaweza kushuhudia hilo, sisi tulio Wakristo, kwamba Yeye yuko pamoja nasi daima. Nasi tunaomba, usiku wa leo, kwamba wenye dhambi waweze kumjua kama Mwokozi wao, kwamba wale ambao sasa wamekuwa Wakristo kwa kumwamini Yeye, kwamba watafute matukio ya kilindi zaidi, ili kuwa na Uzima wa Milele kwa njia ya ubatizo wa Roho, wapate kuwa askari waliojiandaa kwa vita vikuu vilivyo mbele.

6 Tunawaombea wagonjwa na wanaoteseka, ya kwamba hakutakuwa na mtu mnyonge kati yetu ibada itakapomalizika, usiku wa leo. Tujalie, Bwana. Utusikie, tunaomba. Uliona kila mkono ulioinuliwa, Unajua kila haja chini ya mkono huo moyoni. Tunaomba, Baba, ya kwamba utamjalia kila mmoja wao haja yake.

7 Na tutakapoondoka usiku wa leo, jalia tuweze kusema kama wale waliorudi kutoka Emau, baada ya kumtambua na kumwona Yesu aliyefufuka, jalia tuseme, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo aliposema nasi njiani?" Kwa maana tunaomba katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

8 Mwaweza kuketi. Tuna furaha sana kuwa hapa tena, usiku wa leo. Nami ninaona watu wanaleta leso zao, tu—tunatetea hilo.

Tunaamini kwamba Mungu hujibu maombi kwa ajili ya wale walio—walio wagonjwa na wahitaji, na kwamba atazijalia haja za watu wanaomwamini na wataomba rehema.

9 Sasa, tumekuwa na wakati mzuri sana katika kuabudu pamoja nanyi Wakristo, hapa Oregon. Nami nimekuwa nikijaribu kuuweka Ujumbe rahisi iwezekanavyo, lakini bila shaka, hiyo ni kusudi asije mtu yeyote akaukosa. Kuna mafundisho makuu, ya kilindi, ya kiroho Kwake, lakini wakati mwingine huwezi kufanya hivyo mbele ya kusanyiko. Lazima tuudumishe rahisi, ili watoto wachanga wasiukose, kwa sababu ninaamini kuwa tumekaribia sana wakati wa mwisho sana hata hatufai kukosa chochote. Lazima tuhakikishe kabisa kwamba tuko—tuko sahihi, na kufanya yale yaliyo sawa, yale ambayo Mungu ametuamuru kufanya.

10 Na sasa tuna mingine miwili, baada ya usiku wa leo, mikutano ya neema, usiku wa leo ukiwa ni wa tatu. Hiyo inamalizikia Jumapili alasiri, nasi tunatarajia, ninatarajia. Huu ndio mkutano wangu wa mwisho Marekani kwa muda fulani mpaka, nitapumzika kidogo. Huu ni mkutano wangu wa tisa mfululizo, ninachoka sana, bado nina miwili huko Canada kabla sijapumzika. Na kisha nitaenda ng'ambo, Bwana akipenda, huko katika nchi za ng'ambo, ili wao pia, ama, nichukue ziara kote, labda, wakati huu.

11 Nilipata waraka, asubuhi ya leo, kutoka kwa rafiki yangu aliyekuwa hapa, mkutanoni, jana usiku. Kama yuko hapa usiku wa leo, Mungu akubariki, Sam. Nina furaha sana kuwa unaendelea vyema, hapa Oregon. Nilimbatiza jamaa huyu miaka mingi iliyopita. Anaendesha chekechea hapa mahali fulani, kulingana na kadi yake, Sammy Sanders kutoka Milltown, Indiana. Nilimbatiza, nilikuwa nikihudumia Kanisa la Baptisti la Milltown, huko Milltown, Indiana.

12 Uko hapa, Sam? Inua mkono wako, kama upo. Napenda . . . Naam, ninamsikia mahali fulani. Naam. Ati nini? Naam. Loo, loo, nyuma *hapa* ndani. Vema. Bwana akubariki, Sam. Juu huko pembeni. Nakumbuka ile siku, siku ile yenye baridi, nikimpeleka Sam mtoni nikambatize. Jamaa zake walidhani kwamba alipata kichaa, lakini sivyo. Endelea tu kushikilia, Sammy, jamani. Natumai ninaweza kutoka nje kukuona kabla ya ibada kuisha, hapa.

13 Unajua, ni uchovu sana. Inakubidi kukaa chini ya maombi, ukitarajia kuona kile ambacho Roho Mtakatifu angekwambia ufanye wakati wowote. Mnaona? Kamwe hujui la kufanya. Mara nyingi Yeye huniita, "Shuka uende ukasimame pembeni mwa barabara, mtu fulani atapitia hapo, waambie *hivi* kisha uone litakalotukia." Mnaona? Nawe unapaswa kuwa tayari.

14 Na hiyo ndiyo sababu nimekuwa nikijaribu kuudumisha Ujumbe rahisi tu iwezekanavyo. Yale ninayojaribu kufanya . . .

Labda baadhi yenu mnaweza kuwa mnashangaa kwa nini siitishi mistari ya maombi kila usiku. Hili hapa kusudi langu: Kwa kufanya hivi, nataka kujenga imani kwa watu katika Yesu aliyefufuka, ili isiwalazimu kungojea hadi ninii . . . karama maalum ipitie mahali jirani. Mwamini tu Yeye popote ulipo, kwa maana Yeye ni Mungu.

15 Haihitaji mikono ya mwinjilisti, ambayo, hiyo ni sawa, wanaweka imani yao . . . Lakini ibada zinapokwisha . . . Na kila usiku hapa, naona mambo yakitokea, siwezi kuwaita haraka vya kutosha, bila shaka siwezi, yanatukia upesi sana. Lakini mtajua, nikiisha kuondoka, yale mambo, ugonjwa ambao umekuwa nao, umekwisha, unaweza usitambue sasa, lakini umekwisha.

16 Hapa, siku moja, nilikuwa kwenye mkutano, majimbo kadhaa kutoka hapa, na kulikuwa na mama wawili waliohudhuria huo mkutano. Kila mmoja wao . . . Mmoja wao alikuwa jukwaani, huyo mwingine mkutanoni, kwenye kusanyiko. Ndipo Roho Mtakatifu akamwambia yule mama aliyekuwa na ugonjwa mbaya wa tumbo, asingeweza kula hata kidogo, hakuwa ameweza kula kwa miaka mingi, kamwambia, kasema, "Nenda nyumbani, umepona. Yesu Kristo amekuponya."

17 Sasa, angalia anachosema. Usiharakishe kuondoka, ngoja kidogo, uone anachosema. Hiyo ni imani yako mwenyewe inayovuta hilo, lakini basi hivyo ndivyo wewe, wewe mwenyewe, unavyofanya, basi ngoja uone anachokwambia. Unaona, hiyo ni—hiyo ni wakati . . . Kisha hiyo ni . . . Unaposikia hilo likitoka, BWANA ASEMA HIVI, basi andika hilo. Hiyo ni . . . itatokea hivyo. Kwa hiyo lilikuwa limetimia.

18 Nadhani Ndugu Borders amewaelezea. Ninamwachia hilo meneja awaambie jinsi mambo haya yanavyorudishwa, jinsi ya kupata kadi yako ya maombi, jinsi tunavyokuja na kuchanganya kadi hizo na kuzisambaza kwa mtu yeyote anayezitaka hizo, na kisha kuita tu kutoka sehemu tofauti kuninii . . . Hiyo ni kuzuia watu kusema . . . vema, wasipopata namba moja au namba mbili, au mahali pengine hapo, wanatupa kadi yao chini, hawaitaki.

19 Hakuna ajuaye mstari wa maombi utatakapoanzia; Mungu huchagua hilo Mwenyewe. Naye mvulana anayesambaza kadi za maombi husimama mbele yenu kwanza, na kuzichanganya hizo kadi zote pamoja, kisha anawasambazia ku—kulingana na mahitaji yenu. Kwa hiyo unaweza kupata namba moja, useme, "Nitakuwa wa kwanza mstarini." Huenda ukawa wa mwisho, na anayekufuata huenda akapata namba tisini, na anaweza kuwa ndiye wa kwanza. Mnaona, huwezi kujua. Na hiyo inampa kila mtu nafasi.

20 Naye Ndugu Borders huelezea jambo hilo, kisha jinsi ambavyo baada ya hayo maombi yamefanywa juu ya huyu pepo, ugonjwa, ulio nao, na magonjwa yote ni ya ibilisi, ndipo wakati

maombi hayo yamefanywa, haiwezekani isitukie, maadamu unaamini kwamba inatukia. Sasa, ukianza kutilia shaka, "Pepo mchafu anapomtoka mtu, hutembea mahali pasipo maji, kisha anarudi na pepo wengine saba wabaya kuliko alivyokuwa hapo mwanzo." Sasa, enyi watu, angalieni jambo hilo.

21 Wanasema, "Loo, vema sasa, nimekuwa mgonjwa zaidi." Sasa, ngoja kidogo, kama hujatilia shaka, endelea kushikilia, kwa sababu kama ni kitu kama uvimbe au chochote kile, ni kundi la seli, na hizo seli hazina budi kufa, uhai katika seli hizo, kisha hizo seli zinaoza, nayo mapigo ya moyo hayana budi kubeba maambukizi hayo kupitia mkondo wa damu. Mnaona? Ndipo hali yako inakuwa mbaya mara kumi kuliko ulivyokuwa, lakini imani inashikilia pale pale, hata iweje. Hamna budi kufundishwa mambo haya.

22 Mungu akipenda, ninajaribu sasa uinjilisti. Tunajua uamsho umekwisha, kila mtu anajua hilo. Nilitabiri hayo huko nyuma mwaka wa '56 wakati huo utakapoanza kuisha. Billy Graham akarudi, na Tommy Osborn, na hao wengine, Nikasema, "Hili ndilo, Marekani italipokea au ilikatae mwaka huu." Nao wakalikataa, sisi hatungojei kitu ila Hukumu. Sasa, lizingatieni hilo mwone kama Ndugu Branham amesema kweli au la. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Tunaelekea huko, tutalipia yale tuliyotenda, tuna madoido mengi sana kanisani, na Hollywood na kadhalika, Mungu amekasirishwa na kuchoshwa nayo. Yule wa mwisho ataingia baada ya kitambo kidogo, na basi hakuna lingine.

23 Ningependa kuwa na wakati, Mungu akiruhusu, kabla ya wakati wa mwisho, wakati ningeweza kuweka hema katika eneo fulani, na kuja tu kwa namna fulani, na kukaa huko kwa yapata majuma manne ama matano. Kukaa tu huko, ambako ungeweza kuwa na kipindi cha asubuhi, pamoja na ndugu wahudumu tu, na ili waweze kulifundisha kusanyiko lao baadaye. Kisha tukae mle ndani, mtu fulani aombewe, halafu iwe mbaya zaidi, wala asijue ni nini, wamrudishe mtu huyo kwenye chumba cha mafundisho, na kuwajulisha. Wachunguzwe tena kuona kilichotukia. Mnaona? Hapo ndipo wewe . . . Ninaamini tutapata matokeo bora zaidi kwake, namna hiyo. Lakini sasa huna budi kulishika katika siku moja ama mbili usiku, na kuliweka rahisi sana ili kila mtu alishike; ni mchanga kwa makasisi na kadhalika, lakini si umbo la uchanga.

24 Lakini tunataka kuliweka hili mbele ya watu. Hili ndilo kusudi langu, ni kuamini kwamba Bwana Yesu Kristo hajafa, lakini yu hai. Manabii walikuja, wakawaua mmoja baada ya mwingine, manabii na wafalme na kadhalika, waliuawa. Mwana alipokuja, walisema, "Yeye ndiye mrithi, kwa hiyo tutamwua." Lakini walipomwua, alifufuka tena. Kwa hiyo yu hai milele hata milele, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Na kama ningaliweza tu kuwafanya watu watambue hilo, mtaona kitu

kikitokea moja kwa moja hapa ambacho kitaninii . . . kitatikisa nchi nzima.

25 Sasa, kumbukeni, tunapozungumza "kuitikisa nchi," hiyo haimaanishi kutikisa chakula cha mizinga hapa, kuna mamilioni huku na huko kwenye pwani hii hapa wanaokiri Ukristo, hawataona chochote. Hiyo ni kweli. Wakati—wakati Yohana alipokuja, hapakuwapo na moja kwa mia ya watu waliopata kujua alikuwa duniani. Yesu alipokuja, nina shaka kulikuwa na wengi hivyo ambao . . . wa watu walioishi duniani ambao waliwahi kujua Yeye alikuwako. Alitumwa tu kwa wale ambao alikuwa ninii . . . "Wote alionipa Baba watakuja. Wala hakuna mtu awezaye kuja, asipoitwa na Baba Yangu." Mnaona?

26 Kwa hivyo ni kwa kundi hilo tu lililochaguliwa ambalo limeitwa. Ujumbe utaenezwa, lakini utapitia juu yao moja kwa moja. Kama tu alivyosema, "Zingine zilianguka kando ya njia, na zingine *huku*, lakini zingine zikastawi." Basi nyingi ni vijazio tu, kujaza wakati. Mamilioni ya watu wanaokiri Ukristo wataukosa kwa maili milioni moja. Hiyo ni kweli. Yote ni katika utendaji wa Mungu. Sasa, hatutaki kuingia katika utondoti huo, yako hapa katika Biblia, na ni Neno la Bwana hasa.

27 Kwa hivyo jambo likupasalo kufanya wewe, na linipasalo kufanya mimi, ni kutafuta wokovu wetu wenyewe, sio shaghalabaghala tu, inamaanisha zaidi ya kila kitu kilichopo duniani, na chochote kwako. Hii ndiyo nafasi yako, wala usibahatishe ukaikosa. Mbingu ni kuu.

28 Si muda mrefu uliopita, wengi wenu mlisoma katika magazeti kuhusu kule kuhamishwa kudogo nilikopewa na Bwana. Sio kuhamishwa, sitalisema hivyo, linawakwaza watu. Lile ono, ningesema. Nilipaona Mahali hapo, nilikuwa kule. Ninapaswa kujua maono ni nini, nimeyaona tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Nami namwomba mtu yeyote aniambie mahali ambapo moja lilikosea, haliwezi kukosea na iwe ni Mungu. Mungu hawezi kukosea. Mnaona? Si mimi, mimi hukosea wakati wote, lakini Yeye hakosei kamwe. Kwa hiyo anapozungumza, ni kweli.

29 Niliona, si muda mrefu uliopita, nilikuwa nimesimama ukumbini, nikingojea ndege, nami nikaona pale walipokuwa wameingiza kwenye . . . maili moja ndani ya bahari, nao walikuwa wamechukua, kule chini ambako wale samaki, wasio na macho. Nao—nao walikuwa na nuru pale, walikuwa wakionyesha viumbe vya baharini vilivyo na sura ya kutisha sana. Nao hao, baadhi yao walikuwa na mwanga mbele yao. Nami nilikuwa nikiwazia. Mmoja akaja, alionekana kama ninii . . . kitu chenye kofia ya bomba la moshi, sijawahi kuona kitu chenye sura mbaya hivyo. Sasa, kama . . . Kitu hicho hakikuwa na macho, lakini hata hivyo kina hisi nyingine inayokiongoza kutafuta chakula chake.

30 Nami nilikuwa nikiwazia, nilipokuwa nikikitazama hicho, “Vipi kama ningeweza kutumia macho yangu, na kumwacha samaki huyo mdogo ajisalimishe kwangu, kwa hisi yangu ya kuona? Jinsi ningeweza kumwongoza!” Ningeweza kuona chakula chake *hapa* mbali sana na kusema, “Usizingatie rada yako mwenyewe, ama chochote kinachokuongoza, maana inakupasa kukikaribia. Ninaweza kukwambia kilipo chakula chako.” Naye angenisikiliza tu, ili. . . Hisi yangu ya kuona ni kubwa kuliko hisi yake ya vile inavyombidi kujiongoza, jinsi angekuwa bora zaidi, jinsi angeweza kula! Tofauti gani. . . Angekuwa samaki mdogo wa kipekee, lakini angekuwa anafuata hisi ya kuona iliyo bora kuliko hisi iliyomwongoza.

31 Hivyo ndivyo ilivyo kwa Roho Mtakatifu. Laiti tungaliweza kumwacha Roho Mtakatifu, ile Hisi kuu ya Roho Mtakatifu ituongoze, na kutuonyesha mambo yajayo, mbali kupita mambo hayo! Mnaona?

32 Sasa, vipi kama maskini samaki huyo angeninii, hajawahi kuona nuru ya mchana, vipi kama angejaribu kupanda kupitia majini? Asingeweza kufanya hivyo. Yeye ameshinikizwa kwa vilindi hivyo vya bahari, kama angepanda juu angelipuka.

33 Sisi tumeshinikizwa kwa ajili ya dunia. Hatuwezi kwenda. . . Kupanda juu kidogo nasi tungelipuka. Hiyo ni kweli. Lakini sasa, vipi kama maskini samaki huyo angeweza kuwa mimi? Je, ningetaka kurudi kwenye wino huo wa usiku wa manane kule chini, na daima niwe mnyama wa aina hiyo tena, mwenye macho ya aina hiyo, ama, hisi? La, bwana. Ningependa kuwa mwanadamu.

34 Sasa, zidisha hilo kwa milioni mia moja, halafu Mungu hana budi kumbadilisha mwanadamu huyu tuliye. Sisi tumeshinikizwa upya na kupandishwa kwenye Uwepo Wake ambapo ni. . . Hatutaki kamwe kuwa na kitu kama hiki tena, mbali zaidi, tumebadilishwa kutoka kwenye kiumbe hiki.

35 Sikilizeni, rafiki zangu wapendwa, ninyi watu hapa, siko hapa kwa sababu ya kukosa mahali pa kwenda, niko hapa kwa sababu nilijisikia kuongozwa kuja hapa. Huyu hapa meneja na kitabu kilichojaa maeneo, duniani kote. Mnaona? Lakini nilihisi kuongozwa kuja hapa, nilikuja hapa kwa shida. Hawa ndugu hapa, tulipokuwa mkutanoni hivi majuzi asubuhi, natumaini mlipata kile kilichokuwa kikiendelea kwenye hicho kifungua kinywa. Na huko, kwa kuwa walinileta huku kwa shida, huku nikijua hayo hata kabla sijaondoka nyumbani, nikiyaona kwa ono.

36 Nasi tuko hapa kwa sababu Mungu ana jambo fulani hapa. Asubuhi ya leo, yapata saa mbili asubuhi ya leo, nilitwaliwa katika ono, ndipo nikaona, nilikuwa na wasiwasi juu ya mkutano huu, nami nikaona mwanamke akija mbele yangu na kuketi.

Naye akasema, “Ni kizuri sana kupita chochote ambacho tunaweza kuwazia.”

Nami nikawazia, “Ni nini hiki?”

37 Nami nikamsikia akisema nami, akasema, “Endelea tu kujitahidi, usiogope. Endelea kusonga mbele.” Kwa hivyo najua, najua bila shaka lolote. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Kuna jambo linalokaribia kutukia, ama linaloendelea hapa. Ama mtaona uamsho mkubwa ukijitokeza wenyewe, au mtaona hukumu, au yupo mtu ambaye Yeye anamtafuta. Kuna kitu fulani, sijui. Lakini Yeye anafurahia kufanya yale tunayofanya sasa hivi. Endelea kuvuta kila mtu uwezaye, na kujaribu tuwezavyo, hayo tu ndiyo tujuayo. Na kama mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, kumbukeni hilo ni katika Jina la Bwana.

38 Sasa, rahisi, najaribu kulifanya rahisi, kulidumisha hivyo. Hapa si muda mrefu uliopita, mtu mzuri sana wa kidini, mwenye sifa kubwa nchini, basi aliniita chumbani kwake, naye akasema, “Kasisi Branham, ninataka kukwambia jambo fulani.”

Nami nikasema, “Naam, bwana. Endelea.”

Naye akasema, “Napendezwa nawe kama mtumishi wa Kristo, nami naamini ndivyo ulivyo.”

Nikasema, “Asante, bwana. Ninaweza kukupa heshima hizo.” Hatupatani kimawazo, lakini hata hivyo tunatambuana kama watumishi wa Kristo.

Akasema, “Nilikuleta hapa nipate kukuombea.”

“Asante, bwana.” Nikasema, “Hakika ninayahitaji.”

Naye akasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani.” Kasema, “Kwa nini usiache kuwakemea hao watu?”

Nikasema, “Unamaanisha nini, bwana?”

39 Kasema, “Unawakaripia hao wanawake kuhusu kukata nywele zao, kuvaa nguo za kizinifu, na waume wao, jinsi walivyo duni kuwaacha wa-. . . wake zao kufanya mambo kama hayo, na kupayuka namna hiyo.” Kasema, “Hao watu wanakuchukulia kuwa nabii.”

Nikasema, “Uliwahi kunisikia nikisema nilikuwa hivyo?”

40 Akasema, “La, lakini watu wanakuchukulia hivyo.” Kasema, “Unaona, unapaswa kuwa ukiwafundisha watu hao jinsi ya kupokea karama kuu za kiroho, na kuinuliwa juu, na kuwa na mambo ya kimbinguni kama hayo, na madhihirisho makuu ya Roho. Unapaswa kuwa ukifundisha hayo, badala ya kuhusu kukata nywele zao, na kuvaa nguo jinsi wafanyavyo.”

41 Nikasema, “Bwana, iwapo hawawezi kuelewa ABC zao, nitawafundishaje aljebra?” Hiyo ni kweli. Hawana adabu ya kawaida ya kulitii Neno la Mungu! Je, mnajua ABC inasimamia

nini? Sikuzote Mwamini Kristo [Eng. Always Believe Christ—Mfa.], Naye ni Neno. Hiyo ni kweli. Naam.

42 Ni nini kinachowafanya watu kufanya hivyo? Hebu kidogo. Ni nini kinachowafanya watu kufanya hivyo? Ni kwa sababu kwamba unatoa kitu kile kile ambacho Mungu aliweka ndani yako, una kiu ya kitu Fulani, nawe unajaribu kuiridhisha kwa anasa za ulimwengu huu.

43 Mungu alimfanya mtu aone kiu. Alipoumba moyo wake, alimwumba aone kiu kwa sababu alimwumba amwonee Yeye kiu. Basi hebu mtu yeyote athubutu ku—kuridhisha kiu hiyo takatifu kwa mambo ya ulimwengu! Hiyo iliwekwa ndani yako upate kumwonea Yeye kiu, "Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji, nafsi yangu inakuonea kiu, Ee Mungu."

44 Sio kwamba nimelikasirikia Kanisa, ninalipenda Kanisa. Nami najua kwamba—kwamba jambo fulani linakaribia kutokea. Na hiyo ndiyo sababu nasema, "Iweni tayari, enyi watu. Hamwezi kufanya mambo hayo, sura yako ya nje inaonyesha kazi ya ndani ya neema bado haijafanyika."

45 Haidhuru ulipaza sauti kiasi gani, ulinena kwa lugha kiasi gani, ukacheza katika Roho, chochote ambacho huenda umeita mihemuko yako, isipokuwa maisha hayo yaambatane na Neno hili . . . Ati usikie Neno hilo, na kuliacha? Kuna kasoro. Roho Mtakatifu ndani yako siku zote ataliitikia Neno kwa, "Amina. Ni kweli." Mnaona? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo hivyo ndivyo ninavyojaribu kufanya, nikijaribu kutupa kila kitu niwezacho. Ni katika upendo.

46 Eliezeri alipotumwa kutoka kwa Ibrahimu kwenda kumtafutia mchumba mwanawe, Isaka, mfano wa Baba, na Mwana, na mtumishi, na kadhalika, Eliezeri alijitahidi sana mpaka akaikuta tabia. Basi alipoikuta tabia, alifaulu. Na hiyo ndiyo Roho Mtakatifu anayojaribu kutafuta siku hizi, ni tabia. Huwezi kuwa na tabia mpaka uwe na imani, nayo imani huzaa tabia. Basi alipompata Rebeka mrembo . . .

47 Angalieni, alipomjia Isaka, aliufunika uso wake. Kwa nini? Hakuwa na kichwa tena, huyo mwanamume alikuwa ndiye kichwa. Mwanamke anapoolewa, anaweka shela juu ya uso wake. Kwa nini? Anamjia kiongozi wake. Nalo Kanisa, Roho Mtakatifu anapolipata Kanisa, Hilo hujifunika, Kristo ndiye Kichwa Chake, naye Kristo ni Neno. Hajali tena juu ya mapokeo Yake na kadhalika, Kristo ndiye Kichwa Chake. Tabia!

48 Miaka mingi iliyopita, walikuwa na watumwa huko kusini, nao watumwa hao walikuwa na huzuni. Nao waliwauza jinsi ambavyo ungeuza gari la mtumba, huku nje uwanjani, kuwapiga mnada, wanapata hati ya mauzo yao, wanadamu. Hilo si sawa, halijawahi kuwa sawa. Mimi ni mtu wa kusini, lakini haikuwa sawa.

49 Mungu alimfanya mwanadamu, ndipo mwanadamu akafanya watumwa. Hakuna jamii inayopaswa kuitawala nyingine. Sisi ni ndugu, kutoka kwa mti mmoja, Adamu, nasi ni ndugu. Tunaweza kupeana damu, mtu mwekundu, mtu mweusi, mtu wa kahawia, yeyote yule. Sisi ni wanadamu, wala hatupaswi kufanyana watumwa.

50 Lakini walikuja, wakapiga mnada, kisha wanamwondosha huyo mtumwa mkubwa mzito kwa mke wake mwembamba, wakamweka hapa, na kumzalisha na mwanamke mwingine aliyekuwa mkubwa zaidi, apate kuzaa watumwa wakubwa zaidi. Huo ulikuwa ni uovu, kamwe haukuwa sahihi.

51 Siku moja nilikuwa katika jumba la makumbusho. Nilikuwa nikiona, nikipitia kwenye hilo jumba la makumbusho, kulikuwa na mzee mweusi, naye alikuwa tu na maskini mzingo wa nywele nyeupe kuzunguka kichwa chake. Imekuwa kama miaka ishirini na mitano iliyopita, nadhani, labda thelathini. Nilikuwa nikimtazama, jamaa huyu, naye alikuwa akitazama pande zote.

Nashangaa, "Huyu mzee mweusi anatafuta nini?" Alikuwa akitazama pande zote alipokuwa akienda.

Basi muda si muda akafika mahali fulani, akasimama ghafla, akarudi nyuma, akainamisha kichwa chake, na kuanza kuomba.

52 Nilimtazama kwa dakika kadhaa, nikasogea karibu naye. Nikasema . . . Machozi yalikuwa yakitiririka kwenye mashavu yake meusi. Nikasema, "Samahani, Mjomba," kama tunavyowaita . . . hasa sana, ndugu weusi, "Mjomba," Nikasema, "Samahani, Mjomba, lakini naona ulikuwa unaomba." Nikasema, "Mimi ni mhudumu, mimi ni mhudumu wa Kibaptisti, na ningependa kukuuliza kwa nini ukasisimkwa sana. Ni nini kilikusisimua?"

53 Akanitazama, akapangusa macho yake, akanishika mkono, akasema, "Angalia iliyowekwa pale." Nikaangalia chini ya kioo, wala hapakuwa na kitu ila vazi la mwanamke tu, vazi la mtindo wa kale.

Nami nikasema, "Nini cha kigeni hapo, kingekusisimua?"

Akasema, "Bwana, unaona doa lile pale?"

Nami nikasema, "Naam, bwana."

54 Akasema, "Hilo ni doa la damu ya Abraham Lincoln." Akasema, "Ubavuni mwangu kuna alama ya mkanda wa utumwa, damu hiyo iliniweka huru na ukanda huo wa utumwa. Hilo si lingekusisimua?"

55 Nikawaza, "Ikiwa hilo lingesisimua, damu ya Abraham Lincoln, ingemsisimua mtumwa kwa sababu aliondolewa mshipi wa utumwa, Damu ya Yesu Kristo inapaswa kufanya nini kwa Kanisa?" Inapaswa kututupa magotini mwetu kwa machozi; tulikuwa watumwa wa Shetani, akatuondolea huo mkanda.

56 Siku moja, kwenye shamba la kale, mnunuzi alipitia pale. Kuna watumwa wengi, na ingewalazimu kuwachapa kwa sababu walikuwa na huzuni. Waliletwa kutoka Afrika na Makaburu, na kuuziwa watu wa kusini kama watumwa. Na ndipo walipoona kwamba, sikuzote, kwamba . . . Walikuwa na huzuni, hawatawahi kurudi nyumbani, hawatawahi kuwa pamoja na baba, mama, pamoja na . . . hawatakuwa pamoja na mke tena, na watoto. Walikuwa—walikuwa na huzuni, nao ingewalazimu kuwachapa kuwafanya wafanye kazi.

57 Lakini mnunuzi huyu wa watumwa, siku moja aliona pale, kulikuwa na kijana mmoja haikuwabidi kumchapa, kifua mbele, kidevu juu, yuko chonjo wakati wowote. Naye mnunuzi akasema, "Ningependa kumnunua mtumwa yule."

Lakini mwenyewe akasema, "Yeye hauzwi."

Akasema, "Ni nini kinachomfanya awe tofauti sana na watumwa wengine?" Kasema, "Je, yeye ndiye bosi wa hao wengine?"

Akasema, "La, yeye ni mtumwa. Nilimnunua, naye, mtumwa tu."

Akasema, "Vema, labda unamlisha tofauti na hao wengine."

Akasema, "La, la. Yeye . . . Mimi . . . Wote wanakula huko nje, manchani, kama tu watumwa wengine."

Akasema, "Basi ni nini kinachomfanya awe tofauti sana na hao wengine?"

58 Naye mwenye shamba akasema, "Nilishangazwa na hilo kwa muda mrefu, lakini siku moja nikagundua. Huko katika nchi ya uenyeji, yeye ni mgeni hapa, lakini huko katika nchi ya uenyeji, alikotoka, baba yake ndiye mfalme wa hilo kabila. Na ingawa yeye ni mgeni, na katika nchi nyingine, yeye anatenda kama mwana wa mfalme."

59 Mungu aturehemu. Kama sisi ni wana na binti za Mungu, ingawa sisi ni wageni katika maisha haya . . . Mungu anatafuta tabia kutoka kwa wanaume na wanawake wanaoweza kutenda kama wana na binti za Mfalme. Mungu aturehemu, kwamba tutafanya hivyo.

60 Hiyo ndiyo ninayofuatilia enyi marafiki, tabia. Hiyo ndiyo Mungu anayohitaji, tabia ya Bibi-arusi huyo ambaye ataondolewa. Na kama wana na binti za Mungu, na tutende hivyo, tuwe wana na binti. Mungu atusaidie.

61 Nataka kusema jambo fulani. Nataka kutangaza somo langu usiku wa leo. Ndiyo maana ninaliweka rahisi. Sasa, iweni na kicho kabisa, na msikilize kwa dakika chache tu. Pia kumbukeni kusudi langu ni, kwa maombi na imani, kumleta Yesu Kristo, yule Mungu mnayempenda na kumtumikia, moja kwa moja miongoni mwenu.

62 Kwa nini hamwezi kumkubali na kumwamini, wakati Yeye yuko papa hapa pamoja nanyi, pamoja na ahadi za Biblia nyuma yake? Hiyo ndiyo sababu nililifanya jinsi lilivyo, rahisi tu kabisa, ili msilikose. Mnaona?

63 Sasa, wakati Yeye yuko papa hapa pamoja nanyi, akitenda kazi moja kwa moja kupitia kwenu, akijithibitisha Mwenyewe papo hapo pamoja nanyi, kama vile Maandiko yalivyosema Yeye alikuwa, na vile Yeye angekuwa . . . Kile alichokuwa, angali hicho, na atakuwa hivyo milele. Basi mwangalieni akizunguka miongoni mwenu, halafu hiyo . . . kwangu mimi, hilo linapaswa kuwafurahisha hivi kwamba mnge—mngejipenyeza kwa nguvu kupitia kila kutokuamini, mweke kando kila kitu ambacho hakikuwa cha kitauwa, msimame na kufanya maungamo yenu.

64 Grass Valley, si muda mrefu uliopita, majuma machache yaliyopita, nilizungumza juu ya kukosa maadili kwa kanisa siku hizi, na kila mwanamke aliyekata nywele kwenye uwa- . . . akasimama, na wahudumu wakasimama, na kulia wapate rehema. Ndipo Mungu, usiku uo huo uliofuata, akafanya tupu kila kiti, kila kiti cha magurudumu, kila kitanda, chochote kile, na kumponya kabisa kila mtu.

65 Ndugu, Mungu ana masharti unayopaswa kutimiza. Unaona? Inakupasa kuyatimiza hayo. Na ikiwa huwezi kufanya hayo mambo madogo ya duniani, tutawezaje kufika *huku* juu na kufundishwa mambo ya Mbinguni? Kwa hiyo hebu na tuifanye kuwa ya kidunia, mpaka sehemu hiyo imalizike, ndipo tutaingilia ya Kimbinguni.

66 Nitatangaza somo langu kabla sijasoma Maandiko. Somo langu usiku wa leo ni: *Ushuhuda Baharini.* Na fungu langu la maneno usiku wa leo ni: "Msiogope; Ni Mimi." Sasa, kumbukeni, somo langu ni: *Ushuhuda Baharini*, na fungu langu la maneno ni: "Msiogope; Ni Mimi."

67 Sasa, kwenu ninyi mnaotaka kusoma Maandiko, hebu na tufungue Biblia sasa, Neno la Mungu, kila mmoja, aliye na Biblia yake, ninawatakeni, fungueni msome pamoja nami Mathayo, mlango wa 14, na kuanzia na kifungu cha 22.

> *Mara Yesu akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga makutano.*
>
> *Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba: Na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake.*
>
> *Lakini kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana na mawimbi, kwa maana upepo ulikuwa wa mbisho.*
>
> *Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaendea, akienda kwa miguu juu ya bahari.*

Wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu.

Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msiogope.

68 Lazima ilikuwa inachelewa. Walikuwa na mkutano mzuri sana siku hiyo. Jua lilikuwa likitua, likitua katika ziwa dogo la Galilaya. Nao wote walikuwa wamechoka, walikuwa wamedhoofika, siku nzuri sana ya mikutano, watu. Ninafanya hili mchezo wa kuigiza ili watoto waweze kulipata. Basi kila mtu alikuwa amechoka na amedhoofika.

69 Ninaweza kuuona mgongo wenye misuli wa mvuvi huyo mkubwa, huku akikivuta hicho chombo, akikisukuma mbele kupitia kwenye mchanga mpaka akakiingiza majini ili kiweze kuelea chini ya . . . majini, akapanda kwenye demani ya hicho chombo akaketi kando ya nduguye Andrea.

70 Na wote ufukoni, hapana shaka kulikuwa na maelfu ya watu, wote . . . baadhi yao wakipangusa macho yao machozi na kusema: "Rudi. Tuone tena. Mrudisheni tena."

71 Mwajua, kuna kitu kuhusu kuwa na mkutano, kwamba unapokuwa na mkutano mzuri wa kiroho ambapo jambo fulani linaendelea, mambo makubwa yamefanyika, unachukia tu kuwaacha hao watu, nao watu wanachukia kukuona ukiwaacha.

72 Hilo daima limekuwa huzuni kubwa, kwangu, baada ya mkutano mkuu kusema, "Kwaheri," najua kuna wengi hapo ambao sitawaona tena katika maisha haya. Na yale niliyosema yameandikwa kwenye vitabu, itanibidi kukutana nao pamoja na hayo Siku ya Hukumu. Kwa hiyo ninakuwa mwangalifu kwa yale ninayosema, kuyadumisha pamoja na Neno.

73 Sasa, walipokuwa wakichukua makasia yao, na kuanza kuondoka, pengine wangeninii . . . Sasa, siku hizo mashua hazikuwa—hazikuendeshwa kwa mota, kama tulizo nazo siku hizi, wakati mwingine ilikuwa tanga. Walitumia tanga na kasia. Wala haikuwa meli kama tuliyo nayo, kama Biblia inavyoliweka hapa, "katika chombo," lakini zilikuwa mashua kubwa, sana sana kama ma—mashua ya samaki. Nazo zilikuwa na makasia, makasia makubwa mno, na mtu aliyeshughulika na makasia haya ilimbidi ajue alilokuwa akifanya, kwa sababu mawimbi . . .

74 Mtu yeyote anajua kwamba kama ukiingia kwenye dhoruba ziwani, au baharini, huwezi kamwe kuiacha mashua hiyo ijiendeshe yenyewe, na mawimbi, itazama. Unapaswa kujua jinsi ya kuyakamata mawimbi haya, na kuyapanda kwa upande, na kushuka. Ukiipandisha mashua yako moja kwa moja, na kuipandisha juu ya mawimbi meupe, afadhali uwe mwangalifu, itazama, itaenda moja kwa moja, ijae maji. Kwa hiyo lazima ujue jinsi ya kupanda mawimbi hayo kwa mashua.

75 Kwa hivyo basi, kwa kawaida huweka, labda mtu mmoja kila upande, kwenye mashua ndogo. Wakati mmoja walikuwa na wawili kwenye kasia moja, lakini kwa kawaida mtu mmoja kwa kasia kwenye mashua ndogo ya kuvua samaki, kama hii ilivyokuwa, nao walitunza wakati. Halafu basi, walipoingia kwenye dhoruba iliwabidi kujua jinsi hasa ya kuvuta makasia haya kufanya mashua hii ipande mawimbi, ili waweze kuyaabiri.

76 Kisha walikuwa na tanga, wakati pepo zilipokuwa zikivuma, mawimbi hayakuwa makubwa sana, wangeweza kuchukua tanga hili na kulifunga wakati mwingine. Nanyi mnajua jinsi ilivyo, katika kuabiri. Lakini hii ilikuwa laini sana, ilikuwa siku nzuri, na—na maskini hiyo bahari ilikuwa tulivu kwelikweli, hamna wimbi ndani yake.

77 Ilikuwa ni raha jinsi gani kutumbukiza makasia hayo ndani ya maji hayo safi, na kuinamisha migongo hiyo humo, na kwa wakati ufaao tu, kila kasia, ni kama mdundo. Ndipo wangepiga makasia mawili au matatu, kisha mtu fulani angesimama, na wote wakawapungia mkono wa kwaheri, na kuendelea na kuendelea mpaka hilo kundi dogo ufukoni likaanza kuwa dogo zaidi na zaidi; na kwao, maskini hiyo mashua ikawa ndogo zaidi walipokuwa wakiendelea. Hatimaye, wasingeweza kuonana, wakiwa huko nje baharini. Jua lilikuwa likitua sasa, michirizi myekundu tu juu angani kutoka kwenye jua, kutoka kwenye milima ya mbali ya Galilaya.

78 Na ndipo tunaona, walipokuwa wakienda zao, hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana, aliyekuwa mdogo zaidi wa hilo kundi, akachoka. Hakuweza kupiga makasia kama maskini hao wavuvi wakubwa, ambao walikuwa wameishi baharini maisha yao yote, na mikono yenye nguvu, na wamezoea kupiga makasia mchana na usiku.

79 Kijana Yohana, naye, labda katika miaka yake ya thelathini, au ishirini, au thelathini, hapana shaka alisimama na kufuta jasho, akazitupa nywele kutoka usoni mwake, na kusema, "Whiu! Ndugu, hebu—hebu tupumzike dakika chache. Mimi . . . Hii, kidogo inanichosha, nimechoka." Nao wakavuta makasia ndani, hapana shaka walikaa kimya kwa dakika chache, hakuna mtu anayesema lolote.

80 Basi baada ya kitambo kidogo kijana Yohana hapana shaka aligeuka na kusema, "Ningependa kushuhudia wakati tukipumzika hapa." Mnajua jinsi ilivyo mkiisha kufanya mkutano, jambo fulani limetukia, linakuchangamsha, lazima ushuhudie kulihusu. Huna budi kumwambia mtu kulihusu.

81 Hivyo kijana Yohana akasema, "Ningependa kutoa ushuhuda. Hilo ni jambo moja, kwamba baada ya leo tunaweza kusema kweli kwamba hatumfuati nabii wa uongo. Hakika lilikuwa la kusadikisha kwa mtu yeyote, leo, kuona kwamba hatumfuati na-. . . hatumfuati nabii wa uongo, kama vile

walimu wengi, wa siku zetu, wanavyotwambia tunafanya. Tunamfuata Mtu ambaye si mfuasi wa dhehebu lolote kubwa, Yeye anayalaani na kadhalika. Nao wanatwambia kuwa tuko karibu kuingia wazimu, lakini sivyo, kwa maana ninaweza kukumbuka dhahiri nilipokuwa mvulana mdogo. . . " Sasa, tutasikiliza mkutano wa ushuhuda. Hebu tujiunge nao sasa, tukijiwazia sisi wenyewe.

82 Yohana anasema, "Nilipokuwa mvulana mdogo, ninaweza kukumbuka wakati mama yangu angenipeleka ukumbini. Tulilelewa karibu na Yeriko. Na katika majira ya kuchipua, nilipomchumia mama yangu shada la maua, na—nami ningeona macho yake mazuri ya kahawia wakati nikimletea hayo, naye angeniweka mikononi mwake, na kunipembeza, na kuniimbia nyimbo kuhusu Mungu, naye alikuwa akinisimulia hadithi za Biblia. Na jinsi nilivyopenda kusikia hadithi hizo za Biblia!

83 "Naye aliniambia kuhusu, chini tu ya kivuko pale, Yoshua mashuhuri, mwenye nguvu alisimama pale, siku moja, na kuyaamuru hayo maji yarudi nyuma, katika mwezi wa Aprili, maji yalipokuwa yakitiririka. Nayo Yordani ikatulia wakati watu wetu walipokuwa wakiingia katika nchi waliyoahidiwa.

84 "Jinsi ambavyo alikutana na yule Shujaa mkuu, wakati alipouchomoa upanga Wake akisimama langoni. Naye, Yoshua, yule shujaa mkuu, akauchomoa upanga wake kukabiliana na huyo Mtu, naye akasema, 'U nani Wewe? Je, uko upande wetu? Au Wewe, ni adui zetu?'

"Naye akasema, 'Mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana.' Yoshua akaitupa dirii yake ya chuma, akapiga magoti.

85 "Nakumbuka Mama akitwambia, akiniambia, hasa, alipokuwa akinipembeza, akasema, 'Sikiliza, Yohana, mvulana wangu mdogo, sikuzote mwamini Mungu. Siku moja watu wetu walipokuwa watumwa, huko chini Misri, Yehova Mungu mkuu alimtuma nabii Wake kule chini. Wakiifuata, tulifuata, Nguzo ya Moto, watu wetu, nao wakaingia nyikani bila chochote, nguo tu walizokuwa wamevaa. Naye Mungu akateremsha mkate kila usiku na kuuweka juu ya ardhi, nao watu wetu wakala mkate nyikani kwa muda wa miaka arobaini.

86 "Nami nilikuwa na shauku kama mvulana mdogo, Nikasema, 'Mama, je, Mungu ana msururu mzima, mkubwa wa tanuru Mbinguni, na kundi la Malaika wanaofanya kazi ya usiku, kwamba wanaenda kule, na kuoka mikate hii yote, na kushuka chini mbio, na kuiweka chini?'

87 "Angeweza kusema, 'La, mwanangu. Unaelewa kama mtoto. Mungu sio lazima awe na meko ya kuokea. Mungu ni Muumba, na yote yaliyompasa Mungu kufanya ni kunena tu Neno, nao mkate ukaanguka juu ya nchi.'

88 "Na sasa, ndugu zangu," akasema, "leo hii nilipowaona wakimleta mvulana huyo mdogo pale, akiwa na hizo biskuti

ndogo tano na samaki wawili, nami nikamwona akiimega mikate hiyo na kuizidisha kuwalisha watu elfu tano, nilijua huyo hakuwa nabii wa uongo. Ilibidi awe na uhusiano na Yehova Mungu, kwa sababu hapa tena, Mungu yeye yule, tunayemwamini, alikuwa papa hapa, akifanya kazi Zake zile zile tena, alikuwa akiumba mkate. Hapana shaka ni Mungu yeye yule aliyewaongoza watu wetu kuingia katika nchi hii." Hakika.

89 Nataka kuwaulizeni. Mvulana huyo mdogo, labda ametoroka shuleni, akiwa na hiyo biskuti ndogo, ama mbili, mikononi mwake. . . Mnaona, hiyo biskuti ndogo haikumaanisha kitu, ingeweza tu kumshughulikia yeye maadamu alikuwa nayo. Maadamu, ilikuwa mikononi mwake, haikuwa na manufaa sana, lakini mara ilipowekwa mikononi mwa Yesu, iliwalisha watu elfu tano.

90 Nayo imani hiyo ndogo uliyo nayo kwa Mungu, maadamu unaishikilia nafsini mwako, haitakuwa na manufaa sana, lakini mara, ukimpa Yeye, angalia kinachotukia.

91 Iwapo ingetokea kuwepo na mwanasayansi hapa, ningependa kukuuliza: Aliifungulia atomu ya aina gani pale? Haikuwa ni samaki tu, bali ilikuwa ni samaki waliopikwa; sio mkate tu wa ngano, bali mkate uliookwa.

92 Ninaweza kumsikia Yohana akisema, "Nilisimama na kumtazama. Je, mlimwona, jinsi alivyokuwa mtulivu na mnyamavu? Hakuogopa, Yeye alisema, 'Ni ninii ngapi. . . Mna mikate mingapi?'

"Kasema, 'Tuna mikate mitano na samaki wawili.'

"Akasema, 'Nileteeni, kisha myaketishe hayo makundi hamsini kwa hamsini.'" Loo, jamani. Hakusisimkwa, alijua kile hasa alikuwa anaenda kufanya.

93 Naye akasema, "Ndugu, hivi hakuonekana kama Yehova? Je, mliyaona macho Yake, jinsi yalivyokuwa na nguvu, jinsi yalivyoonekana? Alionekana tu kama Yehova." Naye alikuwa ni Yehova, amesimama pale akiimega mikate hii, akiwazidisha samaki hawa na kadhalika, na kulisha watu elfu tano.

94 "Kwa hiyo, ndugu, hatumfuati nabii wa uongo, kwa sababu kama Yehova aliwahi kuwa Yehova, hapana shaka Yeye angali ni Yehova, na ikiwa Mtu huyu ni Kile anachodai kuwa, Mwana wa Yehova, atazifanya kazi za Yehova." Amina. Jinsi ushuhuda huo ulivyokuwa wa busara. Hapana shaka uliwasisimua sana.

95 Na bila shaka ilikuwa ni Simoni, mwajua, sikuzote ilimbidi kuchangia sehemu yake, kwa vyovyote vile, akasema, "Ajabu, Yohana, ninauthamini ushuhuda huo. Hebu niingize wangu sasa hivi. Andrea, sasa wewe tulia tu kwa dakika moja," ndugu yake, huku ameketi kando yake. "Andrea alikwenda kukesha Naye usiku kucha, kesho yake asubuhi, huyu hapa anarudi akiniambia, 'Tumemwona Masihi.'

96 “Sasa, mimi ni msomaji wa Biblia. Ninajua kile Masihi anapaswa kuwa, nami najua kumekuwa na wengi wao wamekuja wakisema, ‘Masihi,’ lakini, na ‘*huyu* ndiye Kristo,’ na ‘wakati ulikuwa umekaribia,’ na kadhalika.”

97 Kama ilivyotabiriwa itakuwa katika siku za mwisho tena, “Wengi watakuja, manabii wa uongo, wakisema wakati umekaribia, nami . . . Masihi yuko huko nyikani na Masihi yuko *hapa*.” Kasema, “Msiamini hilo. Mnaona? Msisikilize hilo.”

98 Sasa angalieni, lakini akasema, “Baba yangu aliniambia mimi pamoja na Andrea, siku moja, ya kwamba Masihi atakapokuja, ingembidi kuja kulingana na Maandiko, Masihi wa Kimaandiko. Ndipo nilipoenda Mbele Zake, siku hiyo, pamoja na ndugu yangu Andrea, anayeketi hapa, Naye akanitazama, usoni, na kusema, ‘Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona,’ nilijua ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi.

99 “Nilijua ya kwamba hatukuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne. Naye baba yangu akanionyesha katika Maandiko, kulingana na Gombo la Kumbukumbu la Torati, ambalo Musa aliandika, kwamba Musa, nabii wetu, ambaye tumeishi mamia haya yote ya miaka waaminifu kwa mafundisho yake, kwamba alisema, ‘Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii miongoni mwenu kama nilivyo mimi. Na itakuwa kwamba mtu yeyote asiyemsikiliza Nabii huyu, atakatiliwa mbali kutoka kwa watu.’

100 “Sasa, nilijua, na baba yangu alinifundisha, kwa Maandiko, ya kwamba Masihi huyo angekuwa nabii. Basi nilipomwona akifanya ishara ya Nabii, nilijua Huyo alikuwa ndiye Masihi.” Loo, jinsi hilo hapana shaka liliwafanyia jambo fulani! Naam.

Naye Filipo akasema, “Ningependa kushuhudia. Je, ni sawa, Nathanaeli?”

Naye akasema, “Vema, endelea, toa ushuhuda wako.” Ndipo Nathanaeli akasema, “Naweza kusema neno kwanza?”

101 Basi kila mtu, mwajua . . . Ndipo—ndipo Nathanaeli akaruka juu. Na—naye akasema, “Kaa chini, unaitikisa mashua.” Mwajua jinsi ingekuwa katika mkutano wa ushuhuda, kila mtu hana budi kusema jambo fulani, mwajua, upesi sana. Kisha akasema, “U—unaweza kushika zamu yako. Lakini keti chini, subiri kidogo. Simama kimya, unaitikisa mashua.” Ndipo akasema, “Basi, keti chini utwambie ushuhuda wako.”

102 Naye akasema, “Wakati Filipo aliponijia, nilikuwa kule nyuma, chini ya mti, nikiomba. Ndipo . . . Nilikuwa nikimwomba Mungu amtume Mkombozi. Ndipo Filipo aliponijia, akasema, ‘Tumemwona Masihi. Tumemwona. Tu—tunajua ni Nani, Ni Mwana wa Yusufu, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu,’ nikamshuku.

103 “Nikasema, ‘Sasa, ngoja kidogo. Hakuna kitu chema kingeweza kutoka Nazareti, kutoka kwa kundi hilo la watu.’

Lakini alinitia moyo, akasema, 'Njoo ujionee mwenyewe.'" Sasa, hilo ni jibu zuri. Usikae nyumbani na kulikosoa, njoo, uchukue Biblia yako, na uichunguze, uone kama ni kweli, kwa maana ni nafsi yako, unajua.

104 Kwa hiyo basi akasema, "Tukaja mkutanoni, na mara tulipofika pale alipokuwa Yesu wa Nazareti, alinitazama moja kwa moja usoni akasema, 'Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!'

"Nami nikasema, 'Rabi, ulinijua lini Wewe?'

105 "Akasema, 'Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.' Nalo lilikuwa la kusadikisha sana kwangu, hilo lilitosha. Nanyi ndugu, nyote mnajua nilichofanya, nilianguka moja kwa moja miguuni Pake, na kusema, 'Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli,' kwa sababu nilijua Kimaandiko Huyo alikuwa ndiye Masihi tuliyekuwa tukimtazamia. Niliijua kwa ishara aliyotwambia."

106 Hapana shaka ilkuwa ni Andrea, akasema, "Hebu kidogo, hebu sote tutafakari jambo fulani kwa dakika chache. Je, mnakumbuka siku ile tulipokuwa tukishuka kwenda Yeriko?"

"Naam, ninaikumbuka."

"Na mnakumbuka jambo fulani la ajabu, alikuwa na haja ya kupitia Samaria?"

"Naam, tunakumbuka hilo."

107 "Naye akapanda kule kwenye mji huu, Sikari, na alipofanya hivyo, akatutuma mjini kununua vyakula, nanyi mnajua walivyotutendea mjini. Nasi tuliporudi pale alipokuwa, tulishangaa, Mwalimu wetu alikuwa amekaribishwa na mwanamke mwenye sifa mbaya."

108 Sasa, katika siku hizo waliwatia alama, ungeweza kuwatambua, siku hizi hawana. Lakini wangeweza kutambua kwamba walikuwa na sifa mbaya, jinsi alivyokuwa akifanya.

109 "Nasi tulishangaa sana, mnajua, ndugu, kwamba Bwana wetu angeweza kushikwa na mtu kama huyo, mtu mwenye sifa mbaya kama mwanamke huyu alivyokuwa. Mbona, hakuwa kitu ila mwa . . . mwanamke wa kawaida tu, wa mitaani. Na huyu hapa Bwana wetu, huko nje peke Yake kando ya kisima hiki, akikaribishwa na mwanamke huyu. Kwa hiyo sote tulishangaa mno."

Nao wote wakasema, "Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli."

110 Kwa hiyo wao . . . Akasema, "Tulizunguka nyuma ya vichaka ili kujua alichokuwa anazungumzia, nasi tukamsikia aliposema: 'Mwanamke, nipe maji ninywe.'

111 "Nasi tukawazia, 'Sasa, si ni ajabu hiyo, kwamba Bwana wetu angeomba usaidizi kwa kahaba?'" Hilo linaonyesha alichokuwa kwangu, alikuwa ni Mungu. Hakika. Anaomba

yeyote, kila mwanadamu, haidhuru uko katika hali gani, "yeyote atakaye." "'Si ni ajabu,' tuliwazia, 'kwamba Bwana wetu angemwomba fadhili mwanamke huyu mwenye sifa mbaya?' Nasi tukashangaa.

"Nasi tukagundua ya kwamba upesi alimjibu, naye akasema, 'Bwana, si kawaida, Wewe ukiwa Myahudi, kuniomba mimi mwa—mwanamke Msamaria.'"

Ndipo Marko akaanza kusema kitu, Andrea akasema, "Tulia kidogo tu." Kwa hiyo basi akasema, "Sikilizeni," kasema, "mnakumbuka alichosema?

112 "Akasema, 'Kama ungejua ni Nani uliyekuwa unazungumza naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Nami ningekupa maji usije hapa kuchota.' Nao wakaendeleza mazungumzo kwa muda kidogo kuhusu dini yao.

113 "Halafu, kwa mara ya kwanza, tulifikiri Bwana wetu alinaswa katika mtego, kwa maana Bwana wetu alimwambia huyo mwanamke, 'Nenda, kamwite mume wako, mje naye hapa.'

"Na upesi akageuka, akamtazama usoni, akasema, 'Sina mume.'

114 "Mnakumbuka jinsi mioyo yetu karibu izimie? Tukawazia, 'Sasa, sasa, kuna kasoro. Hapa Bwana wetu anamwambia mwanamke huyo, 'Nenda, kamwite mume wako.' Nasi tulikuwa tumeona ishara ya Kimasihi juu Yake, na kila kitu, nasi tulijua Yeye alikuwa ndiye Masihi, na hapa . . . tunaona kazi Zake, na kujua Yeye alikuwa ndiye Nabii ambaye Mungu alisema angemwinua. Tulijua alikuwa hivyo, lakini hata hivyo huyu hapa mwanamke anayekana ya kwamba alikuwa akisema kweli." Kama vile tu Sara alikana mbele ya Malaika, "Kamwe sikusema hivyo." Lakini mnaona vile Malaika alivyosema.

Kwa hiyo wakasimama pale kwa muda kidogo tu, naye akasema, "'Sina mume.'

"Ndipo basi Bwana wetu akamtazama moja kwa moja usoni na kusema, 'Umesema kweli.'

115 "Sasa, tusingeweza kuelewa hilo, kwa nini ilikuwa hivyo, hapa dakika moja anasema, 'Una mume,' naye akakana kuwa ana mume, kisha Yeye anageuka na kusema: 'Umesema kweli.'

116 "Basi mnakumbuka jinsi tulivyofadhaika? Ndipo akamwambia, 'Umesema kweli, kwa sababu umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Kwa hiyo umesema kweli.'

117 "Jinsi sisi sote tulivyoshtuka, tuone kile mwanamke huyo angesema. Tunajua alipofanya hivi, Mafarisayo, kanisa, wasioamini, walisema, 'Mtu huyu ni mpiga ramli, Beelzebuli, ibilisi.' Lakini maskini mwanamke huyu katika hali yake, aligeuka, na kumtazama usoni, na kusema, 'Bwana, naona ya

kuwa Wewe ni nabii. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya, lakini u Nani Wewe?'

118 "Naye akasema, 'Mimi ninayesema nawe, Ndiye.' Basi kwa hilo akakimbilia mjini na kuanza kuwaambia watu wa mji huo 'Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?'"

119 Sasa, hilo lingepita moja kwa moja juu ya asiyeamini. Hawangelijua kamwe, walichaguliwa tangu zamani kutokuliamini Neno. Mnaamini hilo? Yuda alisema hivyo, "Watu wa kale, waliokusudiwa hukumu hii tangu zamani," kutokea katika siku za mwisho wapate kutokuliamini Neno la Mungu. Ni wangapi wanaojua hayo ni Maandiko? Hakika, waliokusudiwa tangu zamani na Mungu kuwa wasioamini. Ni hali ya kusikitisha jinsi gani! Wasioamini, hawawezi kujizuia, kama vile Esau asivyoweza kujizuia kuwa Esau, ama Farao kuwa Farao. Ni hali ya kuhuzunisha jinsi gani! Na kama wewe ni mwaminio, usiku wa leo, katika Neno la Mungu, jinsi macho yako yamebarikiwa kuishi katika siku hii, kuuona utukufu wa Mungu, jinsi lilivyomiminwa mioyoni mwetu na Roho Mtakatifu kote ulimwenguni, ikiwa hamjakutanishwa *kikanisa* pamoja, mkafunganishwa pamoja na kanuni za imani na madhehebu, hata hamwezi kusikiliza Neno la Mungu.

120 Ni hali ya kutisha jinsi gani kuwa ndani yake, waliokufa mara mbili, wakang'olewa kabisa, kamwe hawana tumaini la kuokolewa. Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema, wamekufa kabisa hata hawaelewi kitu ila kanuni zao za imani.

121 Angalieni, mwanamke huyo, hakuwa amekufa, alilishika upesi. Alikuwa ni Mbegu iliyokusudiwa Uzima wa Milele tangu zamani. Na mara tu hilo lilipomwangazia, haraka akalishika. Alijua, akasema, "Bwana, tunajua ajapo Masihi, atatwambia mambo haya. U nani Wewe?"

Ndipo akasema, "Mimi Ndiye."

122 Naye akaamini, kisha akaenda na kuwaambia watu mjini, nao wakatoka na kumwalika ndani. Hakulifanya mara moja zaidi, lakini Biblia ilisema walimwamini Yesu kwa sababu ya ushuhuda wa yule mwanamke.

123 Sasa, hayo ni Maandiko kadiri nijuavyo jinsi ya kuyaweka. Yako papa hapa mbele yangu nanyi mnayasoma vivyo hivyo, Yohana Mtakatifu, mlango wa 4 ndipo mnapolipata.

124 Basi, hapana shaka ilikuwa ni Mathayo, alisema, "Naomba nishuhudie. Hivi mnakumbuka siku ile tulipokuwa tukishuka kwenda Yeriko, nasi tulikuwa tunakwenda kule kuwatembelea marafiki fulani? Basi mnamkumbuka rafiki yetu kule chini, Rebeka? Naye ni. . . alikuwa m—mke wa Zakayo. Naye alikuwa ametwambia mumewe alikuwa mfanyabiashara, na jinsi ambavyo alikuwa. . . alikuwa mwenye shaka, kwa sababu alikuwa mshiriki wa sinagogi, nayo sinagogi ilisema ya kwamba

mtu yeyote aliyeamini Mtu huyu kuwa nabii alitengwa na kanisa. Naye alikuwa mwanachama wa mashirika yote ya—ya siku hizo, na hivyo wao . . . alijua kama angewahi kukiri hilo, angefukuzwa.

125 "Lakini Rebeka, mkewe, mwanafunzi wa Bwana wetu, alikuwa mwaminio, naye alikuwa akimwambia wakati wote, 'Zakayo, Mtu huyu, kulingana na Maandiko . . . '

126 "'Loo, huna haki ya kuyafasiri Maandiko, Rabi ndiye anayeyasema.'" Lakini Rabi alikosea. "'Rabi ndiye anayepaswa kutwambia.'"

Angalieni, "Lakini Rebeka akasema, 'Nilisimama, nami nikamwona akifanya kazi, nami ninajua ya kwamba Yeye ndiye yule Masihi. Yeye ni nabii.'

127 "Kwa hiyo asubuhi ambayo Yeye angetokea, hapana shaka Rebeka aliomba usiku kucha kwa ajili ya mumewe. Alitaka aokoke." Hiyo ndiyo njia. Huna budi kuwaombea watu. Maombi hubadilisha mambo.

128 "Kwa hiyo hapana shaka aliomba usiku kucha. Karibu mapambazuko, maskini Zakayo aliamka na kuvaa nguo zake bora kabisa alizokuwa nazo, mwajua, kisha akatoka nje, akamwambia tu Rebeka kwamba alikuwa anaenda kupumua hewa safi. Lakini usiku huo labda Bwana alikuwa akimshughulikia, sawasawa na mawazo na maombi ya Rebeka."

129 Sasa, kama unataka Mungu amwokoe mumeo au mkeo, endelea tu kuwaombea, endelea tu kuomba. Hayo tu ndiyo unayopaswa kufanya, endelea tu kuomba na kuamini. Kama kuna cheche yoyote ya Uzima hata kidogo, Mungu atakingamiza kitu fulani njiani hata wataliona. Ndipo kama wakilikataa, basi hiyo ni juu yao.

130 Lakini angalieni, "Kisha, asubuhi hiyo, alikuwa ameomba sana kwamba jambo fulani litukie ambalo lingemsadikisha Zakayo kwamba Huyu ndiye yule Nabii waliyekuwa wakimtazamia." Wayahudi daima wanaamini manabii wao, naye Masihi alipaswa kuwa nabii, maana Mungu alikuwa amewaambia wasiamini chochote ila nabii. Hivyo basi ilibidi awe Nabii. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

131 "Kwa hiyo basi, asubuhi hiyo Zakayo akatoka nje, nami nawazia Rebeka alicheka tu kifichifichi na kusema, 'Mungu asifiwe, anashuka kwenda huko hakika kama nilivyolala hapa kwenye kitanda hiki.'

132 "Zakayo akaenda, anashuka kule. Naye akafika kwenye lango la mbele ambako alijua Yesu wa Nazareti alikuwa anakujia, lakini kulikuwa na watu wengi sana huko asingeweza hata kumkaribia. Isitoshe alikuwa mfupi kwa kimo. Kwa hiyo akapanda Bababara Kuu ya Utukufuni hadi kwenye Njia ya Haleluya." Kwa kawaida hapo ndipo Yeye anapovukia. "Ndipo

akapanda juu ya mkuyu akaketi." Ukitaka kumwona Yesu, utampata kwenye Njia Kuu ya Utukufuni au Njia ya Haleluya, ama kitu kama hicho. "Kwa hiyo alijua angevuka pale, kwa hiyo akapanda na kuketi juu ya mti huu.

133 "Akasema, 'Nitamwangalia, ndipo atakapopiga kona, nitatoa maoni yangu kumhusu. Siamini Yeye ni nabii yeyote, siamini. Na kwa hiyo, nitapanda tu mti huu, nami nitapata maoni yangu juu Yake wakati Yeye atakapopita.'" Kumbuka, hakuwa amewahi kumwona. "Kwa hivyo akawazia, 'Wajua nini? Anaweza kuniona hapa juu.'

134 "Kwa hivyo ninaweza tu kumwona maskini Zakayo huko juu, akivuta matawi yote na majani karibu yake apate kujificha vizuri, asionekane na mtu. Basi baada ya kitambo kidogo, kelele zikatokea barabarani." Ajabu, popote alipo Yesu kwa kawaida kuna kelele nyingi. "Na hizi hapa kelele nyingi zinakuja barabarani, akasema, 'Naam, hapana shaka anakaribia.'

135 "Naye akaona, akija pembeni, jamaa mkubwa mno, mwenye upara, kasema, 'Samahani, jamani, inawabidi msonge nyuma, Mwalimu wetu amechoka sana. Amekuwa hapa . . .' wengine wakipita.

136 "Sasa, ni yupi kati yao angekuwa Ndiye? Baada ya muda kidogo Jamaa mdogo aliyeonekana mpole akaja hapo, akawazia, 'Ati Huyo ndiye wanayemwita nabii? Huyo ndiye wanayemwita Masihi? Mbona, Yeye si nabii, hebu mwangalieni, hata haonekani kama mmoja wao, hata havalii kama mmoja wao.'

137 "Lakini akatembea kwa utulivu, mpaka akafika papo hapo chini ya ule mti, Naye akasimama, kisha akaangalia juu, akasema, 'Zakayo, shuka; ninaenda nyumbani pamoja nawe leo."

138 "Mnakumbuka yale Zakayo aliyosema alipojiunga na Wafanyabiashara wa Full Gospel, kule chini, baada ya yeye kuokoka? Alisema alipigwa na bumbuwazi wakati, sio tu kwamba Yeye alijua alikuwa huko juu, bali alijua kwamba alikuwa ni nani, kisha kasema, 'Zakayo, shuka kutoka kwenye mti huo; ninaenda pamoja nawe nyumbani.'

"Zakayo akaanguka chini, akasema, 'Bwana, ikiwa nimefanya kosa lolote, niko tayari kulirekebisha.'

139 Jinsi tunavyohitaji Zakayo wengi siku hizi! Wakati wanapoweza kuona madhihirisho, na Uwepo wa Mungu yeye yule aliyeahidiwa katika Biblia, na kuinuka na kuuondokea, taifa hili liko katika hali ya kusikitisha jinsi gani. Ni hali ya hukumu iliyoiva jinsi gani!

140 Na mara nyingi mnasema, "Si lazima nisikilize hilo." Nenda kamsikilize mtu atakayewapigapiga mgongoni, na kuwaacha muishi katika dhambi, kisha ukutane nayo huko ng'ambo

kwenye Kizimba cha Hukumu uone kitakachotukia. Ninyi, ikimbieni ghadhabu ijayo. Tubuni, la sivyo mwangamie.

141 Mungu, anapofanya mambo kama anavyofanya siku hizi, hakuna mahali popote katika Maandiko alipowahi kuutuma huo pasipo Hukumu kuufuata. Kweli kabisa. Nayo hukumu itapiga, hakika kama ninavyosimama hapa jukwaani kama mtumishi wa Kristo. Bila shaka. Ninyi kumbukeni hilo.

142 Ni mkutano wa ushuhuda wa jinsi gani! Loo, jamani. Halafu basi akasema, "Je, mnakumbuka tulipotoka mjini pia?" akasema Yohana. "Tulipotoka mjini, kulikuwa na mzee, kipofu ameketi pale, jina lake Bartimayo. Naye alikuwa ameketi juu ya mwamba, nasi tulikuwa yapata yadi mia moja kutoka kwake, ndipo kutoka mjini kikaja kishindo kikuu. Mnakumbuka jinsi Bartimayo alivyotushuhudia na kutueleza jinsi ilivyokuwa?

143 "Alikuwa ameketi pale akijifunza kuhusu, 'Loo, laiti ningaliishi katika siku hizo wakati manabii wakuu walipotembea katika barabara hii, wakati Eliya na Elisha, huku wameshikana mikono, waliposhuka kwa njia hii, wakienda Yordani wakayatenganishe maji wapate kuvuka! Kama ningaliishi katika siku hiyo, ningalikimbia kwenye haya mango, na kuanguka mbele yao, na kusema, "Loo, nabii mkuu wa Mungu, niombee nipate kuona."

144 "'Lakini, ole, walinipeleka kwenye sinagogi, nikamwuliza kuhani kuhusu hilo, akasema, "Sasa, ngoja kidogo, Bartimayo, wewe ni mzee, kipofu, hakuna kitu kinachoweza kukusaidia. Siku za miujiza zimepita. Kuwa tu mfuasi wa kanisa, nawe utakuwa sawa siku moja, utakapoenda Mbinguni."

"'Lakini mnajua, daima nimewazia moyoni mwangu,' akasema, 'kwamba kama kuliwahi kuwako na Mungu, hana budi kuwa angali ni Mungu.'"

145 Loo, ndugu, jinsi tunavyohitaji watu wengine kama huyo! Na kwa kawaida ni wakati unafikiri juu ya mambo kama hayo, ndipo Yeye hutokea. Yachunguze Maandiko, ni wakati watu wanawazia na kuamini. Wakati unapoamua kukaa nyumbani usihudhurie mkutano wa maombi Jumatano usiku ili utazame *Tunampenda Sucy*, ama baadhi ya hayo mambo ya kipumbavu, ya televisheni waliyo nayo, na kukwepa kanisa, utafanyaje jambo lolote na tabaka la watu kama hao?

146 Mnajua, ndege hutengeneza kiota chao katika majira ya kuchipua mwakani, lakini kama ndege huyo wa kiume hajawa pamoja na huyo ndege jike, hayo mayai hayataanguliwa. Anaweza tu kuyaatamia, na kuwa mwaminifu sana, na kukaa hapo mpaka akonde sana asiweze kuruka kutoka kwenye hicho kiota, lakini kama huyo ndege jike hajawa pamoja na huyo ndege dume, huyo dume, mayai hayo hayataanguliwa, yataozea mumo humo kiotani.

147 Na hilo ni baya kadiri lilivyo leo. Tumewachukua watu kwa maungamo, na barua, na kadhalika, kanisani, ambao hawajui zaidi kuhusu Mungu kuliko Mhotentoti anavyojua kuhusu hekaya za Kimisri. Nasi tumepata nini? Kiota kikubwa kilichojaa mayai yaliyooza, wanaume na wanawake wasiomjua Mungu hata kidogo. Ni wakati wa kukisafisha hicho kiota chote, na kuanzia mimbarani hadi kwa bawabu, na kuwapatanisha watu hao na Mungu, ambaye anajua nguvu za Mungu ni nini, ambaye amezaliwa mara ya pili na Roho Mtakatifu. Kweli!

148 Huwezi kuwafanya mashemasi, nao wameoa mara nne ama tano, na upuuzi wa kila namna kama huo, kwa sababu ni njia ya kujitafutia tikiti ya posho. Ni aibu. Upuuzi huo unakuja moja kwa moja miongoni mwa watu wetu wa Kipentekoste, na katika udhaifu wa ujumbe kuwaacha watu *wajifurahishe* dhambini, na kuendelea, halafu bado wanajiita watakatifu. Tunahitaji uamsho wa kutikisa.

149 Si muda mrefu uliopita nikizungumza na yule mashuhuri, ama, kumsikia akiongea, hasa, mwinjilisti mashuhuri, Billy Graham, alipokuwa huko Louisville, Kentucky. Aliwakemea sana hao wahubiri, nilikuwa nimeketi pale. Dk. Mordekai Hamm, yule aliyemwongoza kwa Kristo, yeye ni rafiki yangu mwema, ndio kwanza aingie utukufuni akiwa na umri wa miaka tisini na kitu, ninii chache. . . yapata mwaka mmoja na nusu uliopita, naye Ndugu Hamm alikuwa ameketi pale karibu nami.

150 Ndipo Billy akasimama pale, akasema, "Enyi kundi la wahubiri wavivu," akasema, "Ninakuja mjini na kukaa huko majuma sita, na nikifanya hivyo nitakuwa na maungamo elfu thelathini." Mnajua, ndivyo wanavyoyaita, naamini hivyo ndivyo wanavyoyaita, "Maamuzi." Maamuzi ni sawa, maamuzi ni kukiri, mawe. Lakini inafaa nini kuwa na mawe ikiwa huna mwashi wa kuyakata katika maumbo ya wana na binti za Mungu?

151 Maamuzi milioni moja yana faida gani, wakati bado *wanajifurahisha* katika dhambi, na kutenda kama kila kitu, na kamwe hawana—kamwe hawana mabadiliko ya moyo? Bado wanavuta sigara, kutafuna tumbaku, kunywa pombe, kunusa ugoro, kuangalia televisheni, wanakaa nyumbani wasiende kanisani, kisha wanaweka jina lao kwenye kitabu, na kujiita Wakristo? Wanaume, wakiwaacha wake zao uani huku wamevaa maskini vitu vidogo vya kale.

152 Hapa, hivi majuzi, niliona maono ya kutisha sana ambayo nimewahi kuona, nilikuwa huko chini kwenye Mkahawa wa Clifton, nami nilikuwa nikimngojea Ndugu Arganbright aje. Na hapa mimi. . . akaja mwanamke. Si—si—sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu. Mimi. . . Alikuwa na kijani kibichi *hapa* ndani, na nyekundu, na rangi zote mbalimbali. Huenda angekuwa mwanamke mwenye sura nzuri, lakini

jinsi . . . Alikuwa na moja ya hiyo mitindo ya kukata nywele kichwa maji, kama yule mama taifa, mwajua, na upuuzi huo wote. Naye huyo hapo alikuwa amesimama hapo.

153 Na mimi—mimi ni mmishenari, nimeona upele, nimeona ukoma, sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu. Nami nilikuwa nikimwendea kumwuliza kama ningeweza kumwombea, kumwambia kwamba nilikuwa mmishenari, na mimi—mimi—mimi nilimhurumia. Nami nilitaka kumwombea huyo mwanamke. Nilidhani yeye . . . Si—sijawahi kuona ukoma juu ya mtu namna hiyo: mwanadamu mwenye macho ya kijani kibichi, bluu, na upuuzi wa kila namna, mwenye rangi ya makucha midomoni mwao ya kutosha kupaka kibanda rangi?

154 Enyi wanawake, kulikuwa na mwanamke mmoja tu katika Biblia ambaye aliwahi kujipaka rangi usoni, naye huyo alikuwa ni Yezebeli, naye Mungu akamlisha kwa mbwa. Kwa hivyo ukiona mwanamke amejipaka hizo, unaweza kusema, "U hali gani, Binti Mlowambwa?" Hivyo ndivyo hasa Mungu alivyomwita; alimlisha kwa mbwa. Kweli kabisa.

155 Tunachohitaji siku hizi ni kutakasa nyumba kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Kweli. Naam. Nami nilikuwa naenda kumwombea maskini msichana huyo. Kama angalioshwa, na kuacha nywele zake ziwe ndefu, angalikuwa msichana mwenye sura nzuri. Basi nikaanza kumwendea, nikamwombee, na hawa hapa wengine wawili wakaja, nikasema, "Afadhali ninyamaze kimya, si—sijui. Jambo fulani limetukia tangu nilipokuwa huku nje."

Halafu basi, ninaona jambo hilo kila mahali sasa. Ni ninii . . . Loo, jamani! Jambo hili linawezaje kuendelea tena? Mungu awakataze kufanya hivyo. Naam, bwana.

156 Sasa, turudi kwenye somo letu. "Asubuhi hiyo Zekaria akasema, ama, Bartimayo Kipofu akasema, 'Nilikuwa nimeketi pale, nikisikiliza, nami nikasikia kelele ikitoka mtaani, na kila mtu alikuwa akimwangukia mwingine. Nami nikamsikia kuhani aliyekuwa ameniambia siku za miujiza zilikuwa zimepita.'" Alikuwa ndiye mkuu wa lile shirika kule chini. "Akasema, 'Nilimsikia akisema asubuhi hiyo, "'Tunashuka kwenda kukomesha upuuzi huu. Hatutakuwa na mkutano kama huo hapa."'" Mnajua, i—ibilisi humchukua mtu wake, lakini sio roho yake, Mungu humchukua mtu Wake lakini sio roho Yake pia. Kumbukeni hilo.

157 "Kwa hiyo alipotoka pale, alisema, 'Tunashuka kwenda . . . Sisi . . .' Nilimsikia kuhani yuyo huyo akitoka nje na kusema, 'Aisee, wewe, wewe unayeweza kuwafufua wafu, tuna kaburi zima lililojaa hao hapa. Njoo ukatufufulie mmoja, tutakuamini.'"

158 Yeye hafanyii vitimbi mtu yeyote. Kumbukeni, hao Warumi walipomweka mahakamani asubuhi hiyo, walimfunga kitambaa

usoni Mwake, machoni Mwake, kisha wakampiga kichwani kwa mwanzi, na kusema, "Tuambie ni nani aliyekupiga, kama wewe ni nabii, tutakuamini." Mnajua Yeye alijua ni nani aliyefanya hivyo, lakini Yeye hamfanyii ibilisi vitimbi, Anafanya kazi Zake ili kumtukuza Baba, alisema.

159 Na Ro—Roho Wake Mwenyewe, leo, sifanyi vitimbi, anamtukuza Mungu tu ili kutimiza Neno Lake.

160 Yesu alisema alifanya mambo haya ili yatimie yale yaliyonenwa na manabii. Na leo anafanya mambo hayo kutimiza yale aliyoahidi angefanya. Si lazima afanye jambo hilo, Yeye angeweza kukuruhusu uingie bila hilo, lakini Yeye aliahidi kulifanya, na hilo ndilo analofanya.

161 "Lakini Bartimayo Kipofu," Yohana aliendelea na ushuhuda wake, "Bartimayo Kipofu, alisema, 'Unajua, sikujua, sikuwahi kusikia habari Zake. Muda si muda mwajua, watu walikuwa wakiyumbishwa, nami nikaangushwa chini na kila kitu. Nami nikasema, 'Kelele hizo zote ni za nini? Ni nini kelele hizo zote? Si—sielewi kabisa. Kelele hizo zote ni za nini?'

"Basi hatimaye, mwanamke mzuri akasema, 'Mzee, kuna nini?'

"Kasema, 'Mama, Nani . . . Kelele hizo zote ni za nini? Mimi ni kipofu, siwezi kuona.'

"'Loo, kwani hujawahi kusikia habari za nabii wa Galilaya?'

"'La, mama, sijasikia,' akasema.

"'Naam, Yesu wa Nazareti. U—unajua . . . Je, wewe ni Myahudi?'

"'Naam.'

162 "'Vema, unajua Biblia yetu inatwambia, Magombo yetu, ya kwamba Bwana Mungu wetu atamwinua nabii kama Musa. Naye atafanya kama Musa alivyofanya.'

"'Naam najua hilo; Huyo atakuwa ni Mwana wa Daudi.'

163 "'Loo, hiyo ni kweli kabisa,' kasema kijana . . . 'Mimi ni mwanafunzi wa mtu huyu.'" Mnajua, wanafunzi wote wa Kristo daima wanataka kuwahurumia wale ambao ni vipofu na wale ambao ni wahitaji. Mkutano unaweza kuja katika ujirani, wataenda wamchukue kila mgonjwa wawezaye, kuwaleta. Mnaona? Watafanya kila ki- . . . Kila mwenye dhambi ambaye wanaweza kumpata, sikuzote watataka kuonyesha rehema.

"Ndipo msichana huyu akasema, 'Mbona, Yeye ni yule Nabii wa Galilaya. Anapitia hapa, na . . . '

"'Unamaanisha Yeye ndiye Masihi?'

"'Hakika, Yeye ndiye Masihi.'

"Kisha akasema, 'Yuko wapi?'

"'Yeye yuko takriban ninii mraba . . .'" Sasa, hapo ndipo wanapokuelekeza, mahali alipokuwa, takriban bloku moja ya mji huko chini barabarani.

"'Vema, Yeye . . .' Bartimayo Kipofu akasema, 'Unajua, mimi ninaninii tu . . . Mimi . . . Amenipita tayari.'

164 "Mamia ya watu wakimfuata, huku mmoja akimtupia tunda lililooza, na kusema, 'Hei, wewe nabii wa Galilaya, kama wewe ni nabii, fanya *hivi*.' 'Hei, tuna mtu mgonjwa huku chini, hebu tukuone ukimponya.' Wengine wakisema jambo moja, na wengine wakipiga kelele, 'Salamu Mfalme wa Wayahudi,' na huyu mwingine akisema, 'Utukufu kwa Mungu mkuu wa Mbinguni, ambaye amemwinua Mwana wa Daudi miongoni mwetu.' Na kila . . . Wengine walikuwa wakiimba, 'Hosana' kwa Nabii, kwa Mfalme, wengine walikuwa wakimdhihaki."

165 Hivyo ndivyo ilivyo. Daima ni umati uliochanganyikana, waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini daima walikusanyika pamoja. Hao hapo, hata wakati wana wa Mungu wanapokuja mbele za Mungu, katika Kitabu cha Ayubu alisema, Shetani alikuwa ameketi miongoni mwao, kweli kabisa, wakati wana wa Mungu walipojitokeza Mbele za Mungu. Bila shaka. Wapo kila wakati. Sasa, na hawa hapa, na mmoja akisema jambo moja, na mwingine.

166 "Naye Bartimayo Kipofu akasema, 'Nakumbuka ya kwamba Maandiko yalisema ya kwamba Mwana wa Daudi, kwamba Musa alisema ya kwamba Masihi huyu, Nabii huyu atakayeinuliwa, angekuwa nabii. Na kama angekuwa nabii, Yeye ataelewa. Ee Yehova, unirehemu, unirehemu. Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.'

167 "Ndipo imani yake ikamgusa Yesu." Haleluya! Imani yake! Kamwe asingeweza kumsikia juu ya umati huo wote uliokuwa ukipiga makelele, baadhi yao wakimsukuma chini, wakisema, "Tulia," na kadhalika. Lakini imani yake ilimgusa. Nayo Biblia ilisema Yesu akasimama kimya. Ninataka kuhubiri juu ya hilo wakati mmoja, *Naye Yesu Akasimama Kimya*.

168 "Naam, Yesu alisimama kimya. Ilikuwa ni nini? Imani ya—ya ombaomba kipofu ilimsimamisha, na kumwuliza alichotaka. Naye akamwambia, 'Kwamba nipate kuona.'

169 "Akasema, 'Imani yako,'" kama alivyomfanyia yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, "'Imani yako imekuokoa. Upate kuona, kwa sababu imani yako imekuokoa.' Akageuka, akaanza kuteremka barabarani.

170 "Bartimayo Kipofu akasimama pale, 'Aliniambia nitapata kuona. Mimi hapa.' Jambo la kwanza, aliona kitu fulani kikisogea mbele ya mikono yake, pale, angeweza kuona mikono yake. Huyu hapa akishuka barabarani, akimtukuza Mungu. Mnakumbuka jambo hilo, ndugu?"

171 Loo, mkutano wa ushuhuda ulikuwa ukichochewa vizuri. Loo, kila kitu kilikuwa . . . Nanyi mwajua, ilitokea ibilisi aliangalia chini ng'ambo ya kilima akawakuta bila Yesu, walikuwa wameondoka bila Yeye. Hapo ndipo ibilisi alipopata nafasi yake, akasema, "Sasa, nimepata nafasi yangu ya kuwazamisha, kwa sababu wameondoka bila Bwana wao."

172 Sasa, hebu niseme hivi kwa upendo, kwa kicho, na udugu: Je, hamfikirii hivyo ndivyo ilivyo siku hizi? Nafikiri ni jambo lile lile, kwamba kwenye wakati wa uamsho huu, makanisa yamekuwa matajiri kupindukia. Wapentekoste hawako tena mitaani wakipiga tari. Hawana ujasiri wa kusimama huko nje na kufanya angalau mkutano wa mitaani, unawaona kwa nadra sana. Hiyo ni kweli.

173 Badala ya kuwa na mhubiri wa kale aliyeokolewa na Mungu, wana namna fulani ya mwanafunzi mwenye akili kutoka shule fulani ya Biblia, akijaribu kujifananisha na ulimwengu. Hivi, wakati Israeli walipotaka kumshutumu Mfalme wao, au, kumkana hadharani Mfalme wao, Mungu . . . ? Ndipo nabii alipowaendea, Samweli, akasema, "Hamninii . . . " Walitaka kuwa kama watu wengine wa ulimwengu.

174 Naye Samweli akasema, "Mungu ndiye Mfalme wenu. Mungu amenituma niwe nabii wenu. Je, nimewahi kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana pasipo kutukia? Je, nimewahi kuwaomba riziki yenu? Je, nimewahi kuchukua pesa zenu?"

"La."

"Je, nimewahi kuwaambia jambo lolote, BWANA ASEMA HIVI, pasipo kutimia?"

"La, Samweli, kila kitu ulichosema kilitimia hasa kabisa. Tunaamini wewe ni nabii wa Mungu."

"Vema, basi kaeni mbali na mfalme wenu."

Lakini wakasema, "Lakini—lakini tunataka kutenda kama akina Jones." Mnaona, walitaka kutenda kama hao wengine.

175 Basi enyi ndugu, kwa heshima zote za kiungu kwa madhehebu yetu, hilo ndilo jambo lile lile ambalo makanisa yetu yanafanya. Yanajaribu kutenda kama hayo mengine, kama Methodisti, Baptisti, Presbiteri na Lutheri, wenye ustaarabu, wagumu, waliovalia nadhifu, kanisa kubwa kuliko yote mjini, miradi mikubwa ya ujenzi. Ni fedheha jinsi gani, wakati mamilioni ya wamishenari wangekuwa hudumani leo hii, na wengi wao, hawafadhiliwi, bila viatu miguuni, wakijaribu kuhubiri Injili. Nasi tunajenga majengo ya mamilioni ya dola, sehemu kubwa, na shule, na kuhubiri, "Wakati umekaribia, Kuja kwa Bwana." Kuna kasoro mahali fulani. Afadhali nininii . . . Nitabaki nyuma na ujumbe rahisi. Vema.

176 Angalieni, kulikuwa na tatizo fulani. Nao hao hapo. Ni wakati wa jinsi gani wa Shetani kuingia!

177 Tulienda kombo na programu kubwa. Mkutano ulianza, pesa zikaingia, kila kitu, "Hatuna budi kuongeza makundi yetu." Kila moja, "Wewe njoo hapa ukajiunge na *hili*," kuongoa, chochote kile, kutengeneza dhehebu kubwa zaidi, kujenga shule kubwa zaidi, kujifunza theolojia, kadhalika. Masalaale.

178 Inakubidi kwenda shuleni kwa muda wa miaka kumi kabla angalau hujatawazwa kuwa mhudumu. Halafu basi, wanafanya nini na wewe huko? Wanatia ndani yako dawa ya kutunza maiti isioze, wanatoa yote ambayo Mungu aliwahi kuweka ndani yako. Hiyo ni kweli. Ni kweli. Mungu alikuwa nao siku kumi tu, na kufanya mengi nao kuliko shule zinavyoweza kufanya katika miaka kumi. Aliweka kitu fulani ndani yao, nayo shule hutoa kile Mungu alichoweka ndani, mara nyingi. Wanajifunza hizo saikolojia, na upuuzi wa aina hiyo yote.

179 Na baadhi ya madhehebu yetu makubwa, katika Pentekoste nasikia, kwamba inawabidi kusimama pale, na kabla mmishenari hajaingia hudumani, anafanyiwa uchunguzi wa akili. Rehema, masalaale. Mngeweza kuona kitu kama hicho? Mungu ndiye uchunguzi wetu; Maandiko ndiyo uchunguzi wetu, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

180 Ikiwa huna Ph. D., LL. D., hata hawatakuruhusu kuingia mimbarani. Hiyo ni kweli. Naye Petro alikuwa mjinga sana hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe, naye Mungu akamfanya kuwa kiongozi wa kanisa. Hakika. Ni tofauti jinsi gani!

181 Nikiwa nimeketi huko Jamaica, majuma machache yaliyopita, ama, miezi kadhaa iliyopita, nilikuwa nimeketi kule pamoja na Wafanyabiashara Wakristo. Tulikuwa na mkutano, na yote waliyokuwa wamefanya usiku huo yalikuwa ni kushuhudia, walipokuwa na watu mashuhuri wa visiwa hivyo, hata baadhi ya watu wa Castro huko juu, na kila kitu, watu mashuhuri. Ndugu zetu wa Full Gospel, ninazungumza kwa niaba yao, ninapendezwa nao, ninawapenda, ni ndugu zangu, sina chochote dhidi yao.

Nilikuwa nimesimama pale, nikasema, "Ninyi watu mlinifanya niuonee aibu Ujumbe niliokuwa nikihubiri."

Nao wakasema, "Mbona hivyo?"

182 Nikasema, "Kitu pekee mlichoshuhudia ni kwamba ulikuwa na biashara ndogo, chini pembeni, ukipata dola mia moja kwa mwezi, na 'Utukufu kwa Mungu, kwa ghafla,' sasa una msururu wa Kadilaka." Nikasema, "Kamwe hamtawahi kujilinganisha na hao watu. Hamwezi kuuingiza ulimwengu, au, hamwezi kujilinganisha na ulimwengu, jambo pekee liwapasalo kufanya ni, sio kujilinganisha na ulimwengu, kama vile makanisa na kadhalika wanavyojaribu kufanya, kwa madoido yao na kadhalika huko nje, hamna budi kuwaalika kwa misingi yenu,

si kutenda kama wao. Acheni waje watende kama ninyi." Ee Mungu, uturehemu. Whiu! Hiyo ni kweli.

183 Sisi hawa hapa katika machafuko ya aina hiyo siku hizi, tumeketi, Kuja kwa Bwana kukikaribia, kila mtu amelala, kama tu Biblia ilivyosema ilikuwa. Sisi hawa hapa katika hali hiyo, Wakati wa Kanisa la Laodikia, wakati pekee wa kanisa wa nyakati zote ambapo Kristo aliwekwa nje ya jengo Lake Mwenyewe, akibisha, akijaribu kurudi ndani tena. Hiyo ni kweli. Wakati wa Laodikia, na huo ndio wakati huu, amewekwa nje na kanuni zetu za imani na mafundisho ya sharti, na kuongezea kwenye Biblia, na kuondoa Kwake, na Yeye huyo hapo amesimama nje akijaribu kurudi ndani. Nalo kanisa mle ndani likifikiri ya kwamba wanafanya jambo fulani, "Wenye mfano wa utauwa . . . "

184 Biblia inazungumza juu ya wakati wa kielimu. Ilisema wangekuwa na mfa-. . . "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiopenda kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wenye kudharau walio wema; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake; hao nao mjieupushe nao. Maana hao ndio waendao na kuwaongoza wanawake wajinga waliochukuliwa na tamaa za kila namna," mambo ya kila namna, wanajifananisha na kahaba fulani wa Hollywood badala ya. . . Kristo ndiye Mfano wetu! Hollywood haina uhusiano wowote nalo, na mitindo ya ulimwengu na kadhalika. Tunahitaji kusafishwa. Mrudieni Mungu.

185 Najua ninawachelewesha, lakini ninafanya hivi makusudi. Angalieni, tutafikia kwenye jambo muhimu, kile ninachotaka kuwaambia.

186 Angalieni, pepo zikaanza kuvuma, bahari ikaanza kuchafuka. Walikuwa wameondoka bila Yeye, walienda kwenye programu kubwa mahali fulani, wakaenda kufanya *hivi*, wote wanavutiwa sana na *hili*, na *lile*, na *linginelo*. Nao walikuwa wameondoka bila Yeye.

187 Umati uliochangamana ulipanda pamoja na Musa ambao ulisababisha matatizo. Nami nafikiri hilo ni kama jambo lile lile ambalo limetokea leo, mambo ya Kimbinguni yamefanyika, nasi tumeingiza kundi lililochanganyikana, jambo lile lile, hilo ndilo linalosababisha matatizo.

188 Angalieni, kisha kule kunguruma, Shetani akaanza kupuliza pumzi yake yenye sumu juu yao: Whiu! Whiu! "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama *hiki*. Unahitaji elimu ya kiakili. Hatuwezi kuwaweka wahudumu wetu mimbarani isipokuwa wawe na elimu kubwa." Nani alisema hivyo? Hilo lilitoka wapi katika Biblia?

189 Kama kwa hao Wafanyabiashara usiku ule, niliwaambia, nikasema, "Mnapata wapi upuuzi kama huo? Wapentekoste wa kwanza walitoka, wakauza walichokuwa nacho, wakaacha

nyumba zao, wakawa maskini, matajiri walifanya hivyo, ili wapate Uzima wa Milele. Na siku hizi, ninyi nyote mnajaribu na kusema mna kiasi gani, wao walijaribu kuona wangeweza kuondoa kiasi gani."

190 Ndipo maskini mwimbaji mmoja kutoka Chicago, ambaye . . . Ndugu . . . Ninasahau jina la huyo Mwitaliano, mhubiri mdogo. Naye akasema—akasema, "Lakini, Ndugu Branham, ninataka kuitisha usikivu wako kwa jambo fulani. Hilo lilikuwa kosa kubwa sana walilofanya."

Nikasema, "Umesema nini?"

Akasema, "Walikosea walipofanya hivyo."

Nikasema, "Ati Roho Mtakatifu afanye kosa, Ndugu?"

191 Akasema, "Vema, walikosea kwa kuuza mali zao. Baada ya kitambo kidogo, machafuko yakatokea miongoni mwao, nao hao watu hawakuwa na mahali pa kwenda."

192 Nikasema, "Sawa kabisa na mapenzi ya Mungu, walienda kila mahali wakilitangaza Neno. Hivi wao . . . ? Wangalikuwa na makazi, wangerudi na kukaa humo, lakini Mungu aliieneza Injili kwa njia hiyo."

193 Mungu hakosei. Anaweza kwa nia ya kiakili, lakini si kwa njia Yake Mwenyewe ya kuwazia. Hakika.

194 Wakaondoka kwa msisimko, sasa, tunaona ya kwamba walipotoka kwa mmoja, wamesisimkwa sana kwa sababu waliona mikate ikitengenezwa, na mambo kama hayo. Wakawazia, "Loo, tunapiga tu makasia hapa," ndipo wakaondoka bila Yeye, "itakuwa sawa."

195 Ndipo muda si muda mwajua bahari ikaanza kuchafuka zaidi na zaidi. Shetani akasema, "Sasa, nimewapata. Sasa, nitamwondosha kila mmoja wao, huku nje baharini."

196 Nayo ikaanza kurushwarushwa, nayo mawimbi meupe, ndipo maskini ile mashua ikajaa maji. Nguzo ya mlingoti ikavunjika, makasia yakavunjika, na hao hapo, wakiiacha ielee vyovyote vile walivyoweza. Walikuwa wakipiga mayowe kwa hofu. Kila wimbi . . . Shetani akiwa ameketi juu ya kila wimbi pale, akimemetesha macho yake yanayometa-meta, na kutokeza meno yake, na kusema, "Nitawazamisha kwenye hayo yanayofuata. Nitawazamisha kwenye hayo yanayofuata."

197 Matumaini yote yalikuwa yametoweka. Lakini mnajua nini? Bado alikuwa akiwaangalia. Biblia ilisema alipanda juu mlimani. Naye alikuwa amesimama pale akiwaangalia, akiona walivyokuwa katika shida. Nina furaha sana kwamba neema bado ingalipo, kama sivyo, sote tungekuwa tumekwisha.

198 Alipotuacha, alipanda mlima mrefu kuliko yote ingaliweza kuwepo, Kalvari. Kisha akapanda juu kupita mwezi, nyota, Jupita, Zuhura, Njia ya Kilimia Cheupe, moja kwa moja, mpaka

Yeye akapanda juu sana hata inambidi kuangalia chini kuona Mbingu. Yeye anaweza kuona kila mahali. “Na jicho Lake liko kwenye shomoro,” najua anaangalia usiku wa leo. Amina. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Anaangalia usiku wa leo.

199 Ilikuwaje, wakati saa ya giza ilipowadia, ambapo waligundua hawakuwa pamoja Naye? Na muda si muda mwajua, Huyu hapa akaja, akiwaendea, juu ya bahari. Ni-. . .? Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia. Na kile kinge-. . . walifanyaje? Walipiga kelele. Walimwogopa.

200 Sasa, sikilizeni kwa makini, ninafunga. Waliogopa, wakaogopa Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, kwa maana kilionekana kama mizuka. Wakasema, “Yeye ni mzuka. Huo ni mzuka ukitembea juu ya maji, hakuna kitu kingeweza kufanya hivyo ila mzuka.” Loo, waliogopa. Basi Matumaini pekee waliyokuwa nayo, waliyaogopa.

201 Hilo ni jambo lile lile usiku wa leo. Tumaini la Kuja kwa Bwana Yesu, kuonekana Kwake miongoni mwa watu, nao wanapoiona wanataka kuiita telepathia ya kiakili, wanataka kuiita upiga ramli, wanataka kuiita kila aina ya ibilisi angaliweza kuitwa, nacho ndicho kitu pekee kinachoweza kuwasaidia. Ile Sauti iliyotoka Kwake ilikuwa ni nini? “Msiogope; jipeni moyo, Ni Mimi.” Ilionekana kama ya kutisha mwanzoni, “Lakini Ni Mimi; msiogope.”

202 Sasa, tumekuwa na mikutano mingi ya ushuhuda, nasi tunaona kile kinachotendeka kwa Kanisa. Msiogope, Yeye angali ni Mungu. Yeye angali ni Mungu tu kadiri alivyowahi kuwa. Je, mnaamini hilo? Ushuhuda ule ule aliokuwa kwao siku ile, tunaweza kuamini Huyo ndiye, akiwa ni ushuhuda ule ule kwetu, leo hii. Hivi hamwezi kuamini hilo?

203 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu sasa. Nataka uombe na kusema, “Mungu, nakutaka Wewe, unirehemu, mimi.” Omba kwa njia yako sasa. Mungu, unirehemu, nirehemu. Msiondoke, tafadhalini msiondoke. Ngojeni kidogo, tutaondoka katika dakika moja. Iweni na kicho kabisa.

204 Baba yetu wa Mbinguni, tunapojituliza sasa, baada ya mkutano wa kusisimua, unaokwaruza, mgumu ambapo nimejaribu na yote yaliyo ndani yangu, Bwana, kutoa ushuhuda wa kile ambacho watu wangeninii . . . walichoona Kwako katika siku zilizopita, kile ambacho wangeweza kushuhudia, na kusema ya kwamba walikuwa wameona yakitukia, na hakika ilikuwa ni Wewe. Ulitimiza Maandiko.

205 Sasa, uliahidi huko kurudi tena, kabla tu ya wakati wa mwisho, liheshimu Neno Lako, Bwana. Lifanye Neno Lako liishi tena. Tafuta moyo fulani hapa ndani ambao Wewe unaweza kuthibitisha Neno Lako kwake, Bwana. Nichunguze, Ee Bwana, unijaribu, unisaidie. Unirehemu, Bwana. Uturehemu sisi sote, sisi ni wahitaji.

206 Ninaomba, Mungu, ya kwamba wanaume na wanawake, hapa usiku wa leo, wasiokujua Wewe kama Mwokozi wao, ya kwamba—ya kwamba wataninii—watapata nafasi moyoni mwao usiku wa leo, wasimame kwa dakika chache na kufanya hesabu, washiriki wa kanisa ambao hawaninii . . . wanaojua. Wanaweza—wanaweza kuyachunguza maisha yao wenyewe, haidhuru wameshuhudia nini, wajiangalie wenyewe na kuona kwamba kuna kasoro, wajichunguze wenyewe dhidi ya Neno la Mungu waone linavyotokea. Jalia sote tujichunguze, sasa hivi, Bwana, tuone mahali tumepungukiwa, kisha tukulilie Wewe tupate rehema.

207 Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, na kila mmoja wenu akiomba. Sasa kamwe hatutawaomba kujiunga na kanisa, jiunge na kanisa lolote utakalo. Lakini tunakuomba hivi, mimi niko usiku wa leo, kama mtumishi wa Kristo: Ikiwa humjui kama Mwokozi wako, nawe ungependa kumjua, na . . . Hamniinulii mimi mkono wako sasa, mnamwinulia Yeye mikono yenu.

208 Sasa, kumbukeni, hivi ndivyo Yesu alivyosema, "Yeye alisikiaye Neno Langu," Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye alisikiaye Neno Langu," nimelisema usiku wa leo dhahiri na rahisi nijuavyo kulisema, "Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele."

209 Hujawahi kuamini ama kulikubali hapo awali, lakini ungependa, Mbele za Mungu, kuinua mikono yako, na kusema, "Sasa ninalikubali, Mungu, ninamwamini Yesu Kristo kama Mwokozi wangu, nami ninamkubali sasa kama Mwokozi wangu binafsi."

210 Nitaanza, jana usiku nilikosa mikono fulani, safu zilizoko mkono wangu wa kushoto, mkono wangu wa kushoto, upande wa kulia wa jengo, unapoingia, mkono wangu wa kushoto, ni wangapi hapo ndani mtamwinulia Mungu mikono yenu (Sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kila mtu akiomba, usiinue kichwa chako, omba.), utainua mkono wako, na kusema, "Mungu, ninakuinulia Wewe mkono wangu na ninataka kukukubali Wewe kama Mwokozi wangu, nirehemu, ninaamini kweli wakati umekaribia, na siko tayari kwenda"?

211 Hivi majuzi usiku niliuliza jambo hilo, huko chini, huko California, mwanamke mwenye umri wa miaka sabini na sita aliinua mkono wake wakati wito wa madhabahuni ulipotolewa, akapokea wongofu mtukufu, akaenda nyumbani, akajilaza juu ya mto wake, akaenda kukutana na Mungu. Miaka sabini na sita, na moja kwa moja kwenye dakika ya mwisho kabisa akaingizwa ndani. Vipi kama hangekuja? Hakuna matumaini. Je, utainua mkono wako na kuchukua huo msimamo utoshelezao kwa yote?

212 Hi—hiyo safu iliyoko mkono wangu wa kushoto, hakuna mmoja humo ndani mahali fulani? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Je, kunaweza kukawa na mwingine

ambaye ungeinua mkono wako? Kwa safu ya katikati hapa, mkono wangu wa kushoto, kuna yeyote katika safu hiyo ambaye angejisikia kwamba humpendezi Mungu, na hujamwamini?

213 Sasa, kuna ninii tu. . .Sasa, kuvuta sigara, kunywa pombe, kufanya uzinzi, kulaani, hizo si dhambi. Kuna dhambi moja tu, hiyo ni kutokuamini. Unafanya mambo hayo kwa sababu wewe ni asiyeamini, kama ungekuwa mwaminio, usingefanya mambo hayo.

214 Kuna mambo mawili tu, mojawapo ni imani, na hilo lingine ni kutokuamini, mojawapo linakumiliki. Na kama una shaka kidogo juu ya Neno la Mungu, kila Neno Lake likiwa ni kweli, basi wewe ni asiyeamini, Roho Mtakatifu hakai ndani yako. Ukipinga Neno moja la ahadi ya Mungu au kulipigia swali, kuna kasoro. Je, unaweza kuinua mkono wako, useme, "Unirehemu, Mungu?" Hebu pasiwe na mtu anayeangalia, acha tu Roho Mtakatifu. Mungu akubariki, Bwana. Mungu akubariki, Mama. Mungu akubariki, dada yangu. Vema. Safu hii ya katikati hapa, mkono wangu wa kushoto, hao ni mmoja, wawili, watatu, wanne pale.

215 Safu, safu ya katikati, mkono wangu wa kulia, naomba uinue mkono wako, useme, "Mungu, unirehemu, nataka kuamini." Mungu akubariki huko nyuma, ndugu yangu. Huenda umefanya mambo mengi makuu, maishani mwako, lakini hayo ndiyo makubwa zaidi uliyowahi kufanya. Mvulana mdogo, yapata umri wa miaka kumi na miwili, akiinua mkono wake. Mungu akubariki, Mwanangu. Biblia ilisema, "Mtoto atawaongoza." Hajaikokota nafsi yake kupitia magazeti ya *Hadithi Ya Kweli*, na kadhalika, na kile kiitwacho "hadithi za kweli." Kuna hadithi moja tu ya kweli ninayojua: ambayo ni ile iliyo katika Biblia.

216 Watu, watoto wadogo siku hizi wanajua zaidi kuhusu David Crockett, kuliko wanavyojua kuhusu Yesu Kristo. Kila duka la bei rahisi lina vitu vya kaoboi vya kila aina, na hivyo ndivyo watoto wadogo wa Marekani humeza siku hizi.

217 Kwenye safu ya mkono wangu wa kulia, huenda kuna wengine hapo utakayeinua mkono wako, useme, "Mungu, unirehemu. Simwinulii mkono wangu Ndugu Branham; ninakwinulia Wewe mkono wangu. Wewe ndiwe unayeuchunguza moyo wangu, ingia sasa hivi"?. . .?. . .Mungu akubariki, mwanangu, hakika, mwingine, wainue mikono yao waseme, "Mungu, unirehemu. Sitaki kuwa na makosa, si utanichukua"? Mungu akubariki, huko nyuma. Mungu anakuona. Mungu akurehemu.

218 Sasa, kwenye roshani, mkono wangu wa kulia, kuna yeyote hapo ndani karibu na safu hii, hapa ndani, ambaye ungeinua mkono wako, useme, "Mungu, unirehemu." Inua mkono wako.

219 Kupitia kwenye roshani kufikia katikati kwangu, *hapa*, wengine hapo ndani ungeinua mkono wako, useme, "Mungu,

unirehemu." Siwezi kuona vizuri sana huko juu. Nilimwona Malaika wa Bwana hapo ndani jana usiku, lakini nisigeweweza kumtaja. Akashuka moja kwa moja chini, mtu fulani akagusa kitu fulani, kisha akashuka chini. Inua mkono wako. Atawaona ninyi, niwaone nisiwaone, Yeye atawaona.

220 Je, kweli una ujasiri kiasi hicho? Je, kuna kitu fulani halisi kiasi hicho kwako, Mwanaume au Mwanamke, ambaye ungeinua mkono wako, na kukiri ya kwamba umekosea, na kuomba rehema? Inua mkono wako. Upande wa kushoto basi, kwenye roshani upande wa kushoto. Mungu akubariki. Mungu akubariki, Bwana. Hilo ni jambo zuri sana. Mungu akubariki, Mama. Hilo ni zuri. Mungu, uturehemu.

221 Mungu Baba, ninawakabidhi mikononi Mwako. Wa—walivunja kila kanuni ya kisayansi. Kulingana na sayansi, nguvu za uvutano zinashikilia mikono yetu chini, kama vile zinavyoweka miguu yetu chini. Kulingana na kanuni zao, mkono wetu hauwezi kuinuka, kwa sababu zinashuka chini, kwa maana uzito na nguvu za uvutano huishikilia chini, lakini watu hawa waliinua mikono yao, inaonyesha ya kwamba wana roho ndani yao inayoweza kuudhibiti mwili, nao wakavunja kanuni za kisayansi, na kuinua mikono yao kwa Muumba, wakasema, "Unirehemu."

222 Sasa, Bwana, ninasema haya Mbele za Mungu, Kristo, Roho Mtakatifu, Malaika watakatifu, jeshi lote la Mbinguni, na kundi hili, uliloahidi, kama hilo lilikuwa aminifu kutoka mioyoni mwao, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ninawakabidhi Kwako, Baba, kama nyara za Neno Lako likidhihirishwa, lililohubiriwa na Roho wa Bwana, nao ni Wako.

223 Waepushe na Hukumu, na utimize mapenzi Yako ndani yao. Wape ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kama hawajawahi kubatizwa kwa ubatizo wa Kikristo, jalia waupokee, Baba. Pia jalia wapokee ubatizo wa Roho Mtakatifu na wawe watenda kazi, kutoka kwa watoto hawa wadogo walioinua mikono yao, hadi kwa walio wakubwa sana, wanaume, wanawake, wavulana, au wasichana, matineja walioinua mikono yao, Mungu awajalie, kupitia Jina la Yesu Kristo.

224 Ninawakabidhi Kwako, Baba, wao ni Wako. Roho Wako ndiye aliyewaita, nilinena Neno Lako, nao wakalisikia, na kuamini, na sasa, wanainua mikono yao kwamba walilikubali, Nawe uliliahidi. Ninataka kukutana nao katika Nchi iliyo bora, ambako hakuna mauti wala huzuni. Na katika Siku hiyo, jinsi tutakavyokumbatiana shingoni na kupiga mayowe kwa furaha, na kukumbuka usiku huu hapa Salem, Oregon, wakati huu mkutano utakapoletwa kwenye turubai ya skrini kubwa ya Mungu, nao wataona mikono hiyo iliyoinuliwa, jinsi watu hao

watakavyokuwa na furaha. Nitashukuru jinsi gani kuwasilisha hizi kumbukumbu Kwako. Tujalie, Baba, hao ni Wako. Katika Jina la Mwanao, Yesu Kristo. Amina.

225 Sasa, katika utulivu na katika Uwepo wa Mwenyezi, bado tuna kama dakika kumi. Hebu . . . Tusingeweza kuita kadi nyingi mno za maombi. Kesho u-. . . Nitaingia tu na kuita kadi za maombi, Bwana akipenda. Ninawatakeni mwamini bila kadi za maombi. Nitafanya jambo lingine, katika dakika moja.

226 Lakini ni wangapi, katika jengo hili, ambao hawana kadi ya maombi, na mnaamini kwamba Yesu Kristo ndiye Kristo yeye yule niliyetoa huo ushuhuda baada ya ushuhuda, niliwafanya hao wanafunzi kushuhudia jinsi walivyojua Yeye ndiye Kristo, na Waebrania 13:8 inasema, "Ni yeye yule jana, leo na hata milele," ni wangapi wanaoamini kwamba una imani ya kutosha kugusa vazi Lake? Inueni tu mikono yenu juu, mseme, "Niombee, ninaamini," ninyi ambao hamna kadi za maombi, ambao hamna kadi za maombi.

227 Sasa, tafadhalini, iweni na kicho, kwa muda kidogo tu zaidi. Najua ku—kumechelewa, lakini hakujachelewa kupita kiasi, ni dakika ishirini mapema kuliko tulivyokuwa jana usiku, lakini iweni tu na kicho. Sasa, ombeni. Kila mmoja ainamishe tu kichwa chake, kwa njia yake mwenyewe, na kisha uombe huku nikiangalia, nikijikabidhi kwa Mungu.

228 Ikiwa unapendezewa na Mungu na wokovu wako, na kuona ishara na maajabu ambayo nimesema, hapa katika Biblia, kwamba alifanya, nawe unataka kujua kama Yule unayekiri imani yako kwake . . . Nawe uliyeinua mkono wako muda mfupi uliopita, na aje, usiku wa leo, kwa ajili ya wito huu wa madhabahuni, na kukuthibitishia ya kuwa Yeye ndiye Mwokozi wako, ya kuwa anaujua moyo wako, na Yeye ndiye aliyesema nawe, Naye Ndiye anayeweza kujibu sasa.

Iweni tu na kicho. Ombeni tu. Usiwe na shaka. Nakuomba uinue kichwa chako kwa muda kidogo.

229 Petro na Yohana wakipita katika mlango uitwao Mzuri, walisema, "Tutazame sisi." Hiyo . . . Si kwamba walikuwa kitu; cha kuvutia. Sasa, ulikuwa unaungama kwa Mungu, ukiombea shida fulani. Sasa, amini, kwa moyo wako wote sasa. Kuwa macho. Roho Mtakatifu hushituka upesi sana. Ni wangapi wanaojua hilo? Hushituka upesi sana, kamwe hatavumilia chochote kibaya. Kwa hiyo mara akiita, jibu upesi. Omba tu, amini.

230 Sasa, Biblia ilisema kwamba "Yesu Kristo ni yeye yule jana na hata milele. Naye, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Unaamini hilo? Vema, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, kama ungemgusa, Yeye angetenda jinsi alivyotenda jana, siku ile, wakati alipokuwa duniani. Je, mnaamini hilo? Hakika.

231 Mnaona, yule mwanamke aligusa vazi Lake, kisha akaondoka na kuketi, Naye akasema, "Mtu fulani alinigusa Mimi." Akatazama pande zote mpaka akamwona yule mwanamke, akamwambia shida yake ilikuwa nini, nayo imani yake ilikuwa imemponya. Sasa, Yeye ni yeye yule leo.

232 Tafadhalini, tafadhalini, msisogeesogee. Sikemei, lakini angalieni, mnaona, hivi ndivyo ibilisi anaendelea kuniambia, "Hawakuamini wewe la sivyo wangekusikiliza." Mnaona?

233 Mnakumbuka alichoniambia kule Green's Mill? Ni wangapi humu ndani . . . waliokuwa hapa nilipokuwa hapa mara ya kwanza? Vema. Mnakumbuka nikiwajia, nami nikaunyosha mkono wangu, nanyi mngeugusa mkono wangu, nami . . . halafu kama ningetulia tu, pasipo kujaribu kutumia mawazo yangu mwenyewe, angekwambia shida yako? Mnakumbuka hilo?

234 Mnakumbuka niliwaambia ya kwamba Yeye aliniambia ya kwamba ingetukia kwamba ningejua siri yenyewe ya moyo wao? Mnakumbuka nikiwaambia hilo? Sasa inua mkono wako, kama unakumbuka nikisema kwamba kile . . . kwamba Yeye aliniambia kama ningekuwa na kicho sana . . . Mnaona, haya basi. Sasa, imetimia. Mnaona? Kwa hivyo hiyo inalifanya kuwa kweli.

235 Biblia ilisema, "Akiwapo miongoni mwenu mtu wa rohoni, au nabii, na yale asemayo yanatimia, basi msikieni; yasipotimia, basi msimwogope, kwa maana mimi siko pamoja naye." Hiyo si zaidi ya akili, mnaona, kwa sababu kama Mungu yuko atalifanya kuwa kweli.

236 Sasa, ninyi ombeni tu msio na kadi za maombi. Ninyi mlio na kadi za maombi, Mungu akipenda, nitawaweka mstarini kesho usiku, hapa juu, jukwaani, wasio na kadi za maombi. Iweni na kicho kabisa, "Wale wamngojeao Bwana wataninii . . . "

237 Vema, Yeye yuko hapa sasa. Je, mmewahi kuona hiyo picha Yake, ile Nguzo ya Moto, Nuru? Nitakapokutana nanyi kwenye Kiti cha Hukumu, Hiyo haiko umbali wa futi moja kutoka mahali ninaposimama sasa hivi. Hiyo ni kweli, Yeye yuko hapa. Angalieni kama Yeye si Kristo yeye yule. Angalieni kama huyo ni Roho Wake au la. Wewe omba. Gusa vazi Lake, useme, "Bwana Yesu, nijalie nikuguse. Zungumza kupitia Ndugu Branham, itanithibitishia ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

238 Siwezi kufanya . . . Naam, naona mwanamke ndio kwanza ainamishe kichwa chake, papa *hapa*. Hiyo hapo ile Nuru moja kwa moja juu ya maskini mama huyo. Angalia huku, *hapo* nyuma, Mama, wa pili unayeketi, *hapo* nyuma. Unasumbuliwa na ugonjwa wa tumbo, shida nyingi. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Je, unaamini? Maskini mama huyo aliyeketi, wa pili ndani, kichwa chake kingali kimeinamishwa. Kama

ataamini kwa moyo wake wote, anaweza kuwa nayo. Je, unaamini hilo? Uliikosa. Imekuondokea. Aibu kwako.

239 Iko juu ya maskini mama *huyu* anayeketi *hapa*. Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, ama, mtumishi Wake? Mama huyo anayeketi moja kwa moja katika . . . ? . . . Unaamini? Maskini mwanamke mdogo mwembamba anayeketi hapo karibu na huyo mwanamume, mume wake. Wewe amini kwa moyo wako wote. Unasumbuliwa na ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Hebu nikwambie jambo fulani kukuhusu. Una ugonjwa wa moyo mbaya sana, mpaka inawabidi kuweka oksijeni ndani ya nyumba, uwe umepatwa nao ama la. Sasa, hiyo ni kweli, Bwana, unajua hilo. Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Unaweza kupata uponyaji wako, ni juu yako.

240 Kwani watu hawa wana shida gani? Si ajabu mmekufa. Sikuzote mtakuwa hivyo. Kuna ganzi ya roho yako. Hivi huwezi kuamka kwa Kristo? Usiruhusu wasio na hatia wateseke kwa ajili ya wenye hatia, Mungu. Neema na rehema zimetolewa, na bado hata hamzitambui, mtafanya nini?

241 Mama anayeketi papo *hapo* anaonekana kuwa na imani, akinitazama moja kwa moja, anaugua kisukari, kisukari. Huenda asinielewe vizuri kwa sababu yeye ni Mskandinavia, Mdeni. Unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu, Mama? Asante. Asante, Mama. Wewe amini kwa moyo wako wote na kisukari kitakuacha. Wewe hutoki hapa kwa vyovyote vile, wewe si wa hili kundi hapa. Unatoka huko Oregon, lakini uko kwenye Mto Columbia, hiyo ni kweli, mahali panapoitwa Dalles, ama kitu kama hicho. Um-hum. Jina lako ni Bibi Lund. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Wewe likubali, na uamini, nayo yatakwisha.

242 Kwani hili kanisa lina shida gani kwa vyovyote vile? Mtu huyo anayeketi *hapo*, akinitazama, kutoka Eugene, ana ugonjwa wa macho na masikio. Kama wewe . . . Hiyo ni kweli, Bwana? Simama kwa miguu yako basi, ukubali uponyaji wako. Je, una kadi ya maombi? Huhitaji yoyote. Yesu Kristo anakuponya kwa imani yako.

243 Kanisa lina shida gani? Je, limekufa ganzi kwa Injili? Haleluya! Hebu tumsifu Yeye. Haleluya! Asante, Bwana Yesu. Jinsi tunavyokusifu kwa wema Wako! Wewe uliyeinua mkono wako, muda mfupi uliopita, na unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu, njoni hapa chini na hebu tuwe na maombi mafupi pamoja. Toka moja kwa moja kitini mwako, kila mmoja uliyeinua mkono wako, nawe ambaye—ambaye unafikiri kuwa huko sawa na Mungu, Mbele za Mungu njoo hapa chini sasa, na usimame hapa madhabahuni. Hebu tuwe na maombi mafupi pamoja. Kila nafsi inayotaka kuokolewa, njoni sasa.

244 Ndivyo hivyo. Hiyo ni kweli. Tokeni kwenye roshani huko juu, Uweponi mwa Kristo. Inatupasa kuivunjilia mbali roho

hii ya kale, baridi humu ndani, ewe rafiki. Hatutawahi kuwa na mkutano mpaka tutakapokivunjilia mbali kitu hiki kitoke hapa. Kuna—kuna—kuna kutokuamini kwingi sana kwa ibilisi hapa. Hiyo ni kweli kabisa. Kimbia kwa ajili ya maisha yako, mwendee Kristo upesi uwezavyo. Jambo fulani litatokea. Hukumu italifuata hili. Je, hamwamini hilo? Mwondoe huyo ibilisi baridi, wa kawaida anayejaribu kukufunga. Hebu kila nafsi ambayo haiko sawa na Mungu, izunguke madhabahu hii sasa hivi. Mbele za Mungu, ninawaita katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Njoni sasa.

245 Mnaujua ule wimbo, *Loo, Kwa Nini Isiwe Usiku Wa Leo?* Mnalijua pambio hilo? *Loo, Kwa Nini Isiwe Usiku Wa Leo?* Tuambie wimbo fulani ambao nyote mnaimba kama wito wa madhabahuni, Bwana. (Mwingine? Hiyo ni sawa. Tuna njia ya kale ya kusini ya kufanya hivyo. Vema, tupe wimbo wa wito wenu wa madhabahuni.) [Ndugu mmoja anasema, "Ningeenda wapi, ningeenda wapi ila kwa Bwana?"—Mh.] Tutaimba wimbo wa mwaliko, wakati watu hawa wa thamani wanakusanyika hapa.

246 Marafiki, ninazungumza nanyi katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Huenda umefanya mambo mengi maishani mwako ambayo yamekuwa mazuri, hapana shaka umeyafanya. Lakini hii ndiyo hatua kuu zaidi ambayo umewahi kuchukua, ni kumjia Kristo. Hiyo ni kweli kabisa.

247 Tunapoimba sasa, ninataka kila mtu hapa ndani, ambaye hayuko sawa na Mungu, apate. . . aje kwenye madhabahu sasa hivi. Njoo hapa upate kuwa sawa na Mungu, na uondoe ubaridi huo kwako, ujiondolee kutokuamini huko.

248 Kwa nini unaogopa? Yesu angalikuwa amesimama hapa, usiku wa leo, angesema, "Usiogope; Ni Mimi." Je, hivyo si ndivyo alivyofanya alipokuwa hapa hapo awali? Angalia neema ya Mungu wakati hao watu wasingeikubali. Labda watakufa na shida hizo. Naye Huyo hapo akatoka moja kwa moja, akapitia kwenye kusanyiko, na kuwavuta kwa vyovyote vile, kuonyesha ya kwamba Yeye ni Mungu. Bila shaka. Vema, na tuimbe.

. . . ningeenda, ningeenda wapi?
Nikitafuta kimbilio kwa ajili ya nafsi yangu?
Nikihitaji rafiki wa kuniongoza hata mwisho,
Ningeenda wapi ila kwa Bwana?

Ningeenda wapi?

249 Hivi hutasimama sasa na uje? Unaweza kwenda wapi kwingine? Ati uende kwa kanisa lako? Litaangamia pamoja nawe. Ati uende kwa marafiki zako? Watakufa, na kuoza kama utakavyooza. Ati uziendee kanuni zako za imani? Mungu atazipuuza. Njoo kwa Kristo, njoo Kwake, ndipo una Uzima wa Milele. Kumjua Yeye ni Uzima, kumjua Yeye. Na Uwepo Wake, wakati Yeye yuko hapa akithibitisha Yeye ni Mungu yeye yule aliyekuwa pamoja nao huko nje, usiku ule. Si uje? Mara nyingine

tena tutaita. Njoo sasa. Ikiwa kuna hukumu yoyote, maishani mwako, njoo.

Nikitafuta kimbilio kwa ajili ya nafsi yangu?
(Hivi ndivyo utakavyofanya.)
Nikihitaji rafiki wa kuniongoza hata mwisho,
Ningeenda wapi ila kwa Bwana?

250 Sasa, wakati watu hawa wangali wanakuja, ninataka baadhi yenu ambao ni ninii kweli . . . na kwenye misingi ya kuomba pamoja na Mungu, nataka baadhi yenu wachungaji, mshuke hapa sasa, pia ninataka wachungaji, na wanawake wale Wakristo wanaomjua Mungu, waje karibu na wanawake hawa hapa. Ninyi watu mnaomjua Mungu na mnawajali watu . . .

251 Mnajua kile Biblia ilichosema? Katika siku hizi za mwisho unabii ulisema kwamba watu wangekuwa baridi sana na wasiojali . . . Ndipo Roho Mtakatifu aje, kuwatia muhuri wale tu waliougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini. Ninataka kila mmoja wenu wahudumu anionyeshe, mimi, katika kusanyiko lenu, mtu yule anayeugua na kulia, mchana na usiku, kwa ajili ya dhambi za watu mjini. Je, unaweza kuweka mkono wako juu ya mtu huyo? Pia kumbukeni, Roho Mtakatifu ameagizwa kuwatia muhuri hao tu. Asiwaguse wengine, wataangamia.

252 Kwa nini unaigiza kanisa? Hakuna haja ya michezo. Usimchezee Mungu. Mungu si chombo cha kuchezea; Yeye ni Mungu. Sasa, ninyi mlio na nguvu za kutosha na mnaamini, na mnataka kuona nafsi zikiokolewa, njoni karibu na hapa, simameni karibu na wanawake hawa, ninyi wanawake; na kuwazunguka wanaume hawa, ninyi wanaume ambao kweli mnamjua Mungu, na mnataka kuona nafsi zikiokolewa, na mnataka kuona uamsho, mnataka kuona jambo fulani likitukia. Njoni msimame karibu nao sasa, na hebu tuwaonyeshe ya kwamba tunawapenda, nasi tunataka kumwona Mungu akiwaokoa. Ndugu wahudunu, ingieni moja kwa moja kati yao. Hiyo ni kweli. Haleluya!

253 Sasa sikilizeni, nataka kuzungumza nanyi wanapokuja. Iweni na imani. Njoo hapa juu, "Yeye atakayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu." Sasa, wewe kiri kile unachoninii . . . mahali umezembea, jinsi ulivyo mvivu, jinsi umempuuza Mungu, kiri hilo kuwa kosa, na kusema kwamba "Samahani, Mungu, kwamba nilifanya hivyo." Tafuta fadhili Kwake, kisha uangalie yale atakayokufanyia. Kiri tu kwamba umekosea, Naye atayashughulikia hayo mengine yote.

254 Sasa, hebu tuache kusanyiko lote tuinamishe vichwa vyetu. Na kila mtu, popote ulipo, kama unawajali watu hawa, omba, kila mtu sasa. Karibieni, ninyi nyote hapa, na muweke mikono yenu juu ya mtu fulani aliyesimama hapo.

255 Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru sana kumwona Roho Mtakatifu, katika hii saa ya neema na ufahamu, akivunja pingu za kutokuamini, akivunjilia mbali na kutikisia nguzo zenyewe za kuzimu machoni pa ibilisi, kumpofusha kutoka kwenye Injili, na hata hivyo anavuka hayo na kuzichukua nafsi hizo na kuziingiza ndani.

256 Wewe ungali ni Mungu, Wewe ungali Yesu, Yule aliyefufuka. Tunakushukuru kwa ajili ya hawa, wamesimama hapa, wao ni watoto Wako, kuna jambo moja tu wanaloweza kufanya, ni kuja na kukiri kwamba wamekosea, "Naye atakayeungama dhambi yake atapata rehema; afichaye dhambi yake hatafanikiwa," ulisema hivyo, Mungu. Nami naomba, Mungu, ya kwamba utaivunja ile roho ya kale, baridi, ya kawaida inayojaribu kuushika mateka uamsho huu. Tunachukua mamlaka juu yake katika Jina la Bwana Yesu, na kuzivunja nguvu za Shetani kwa Injili ya ufufuo, na Uwepo wa Yesu Kristo katika saa hii ovu, yenye giza.

257 Shetani, waachilie hao watu, toka ndani yao. Wewe ni mshindwa, na hakuna hata mmoja ambaye Mungu amemkusudia Uzima ambaye unaweza kumshikilia, watakuja kwa vyovyote vile, haidhuru unafanya nini. Wanakuja kwa vyovyote vile, Mungu alisema wangekuja, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu; wala hakuna hata mmoja wao anayepotea."

258 Ninaomba, Mungu, ya kwamba utasikia sasa, na kumfanya Shetani, yule mwovu, awaachilie watu hawa. Fanya kila moja ya makazi yao . . . ? . . . waokoe wapendwa wao, mioyo yao na ishike moto.

259 Jalia waombe usiku kucha, usiku wa leo, siku nzima kesho, jalia kuwe na jambo kama hilo litakalotendeka, mpaka kutikiswa kwa Roho Mtakatifu kutaanzisha uamsho mioyoni mwao, nyumbani mwao, katika makanisa yao, katika jamii. Tujalie, Bwana. Tunakupenda, tunakuamini, kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu. Wamekiri kwamba wamekosea, wamekiri kwamba wamefanya makosa, wamemimina nafsi zao Kwako, Bwana. Uliahidi katika Neno Lako kwamba utawaokoa. Uliahidi, na Wewe ndiwe . . . ? . . . Tujalie, Bwana. Wape wokovu . . . ? . . . adui . . . ? . . . Tujalie, Baba, katika Jina la Yesu . . . ? . . .

260 Kila mmoja wenu, anayesimama hapa, anayekubali kwamba Mungu amekusamehe dhambi zako na kutokuamini kwako, inua mkono wako, useme, "Ninakubali, nahisi moyoni mwangu kwamba Mungu ananisamehe." Inueni mikono yenu, kila mmoja wenu, mkisimama hapa. Ndivyo hivyo. Kote kote, vema.

261 Sasa, papo hapo mahali umesimama, pokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Inamisheni vichwa vyenu. Ninyi mlio na Roho Mtakatifu, Biblia ilisema, "Wakaweka mikono juu yao, naye

Roho Mtakatifu akaja . . . ?. . . ” huku mmesimama hapa, hapa ndipo mahali pa kumpokea Roho Mtakatifu. Amina.

Kila mmoja aombe. Kila mtu huko nje kwenye kusanyiko msininii . . . Inamisha tu kichwa chako, omba, uwe mwaminifu . . . ?. . . Omba maombi . . . ?. . . Mungu awabariki.

Ee Mungu, tujalie, Bwana Yesu. Uturehemu, Mungu mpendwa . . . ?. . . Utujalie, Bwana, uturehemu. Jalia Roho Mtakatifu ashuke.

62-0720 Ushuhuda Baharini
National Guard Armory
Salem, Oregon Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org